# *Sauti Isiyojulikana*

Asante, Ndugu Sullivan. Mnaweza kuketi. Ni vigumu kwangu kujielezea kumshukuru Mungu jinsi nilivyo na shukrani kurudi hapa katika maskani hii, usiku wa leo. Kwa muda mrefu nimekumbuka ziara niliyokuwa nayo mara ya mwisho hapa pamoja na Ndugu Sullivan, na hawa watu, na jinsi ambavyo Bwana alitubariki, Jumapili moja asubuhi kanisani.

2 Ndipo nilipokuja tu huku dakika chache zilizopita, na kuwasikia hao watu wakiimba, "Shangwe moyoni mwangu, na amani niani mwangu," huo ndio Wakristo huimba, yale Wakristo wanayoweza kuzungumzia, kuwa na furaha moyoni mwao, na amani niani mwao, wala hakuna kitu kinachoweza kufanya hivyo ila Mungu.

3 Na inaonekana ni vema kurudi huku juu kutoka kwenye moshi-moshi wa California, ambako unaweza kupata pumzi nzuri ya kina mara moja moja. Ambako . . . Wanaweza kuchukua California yote kwa upande wangu. Nami ninawapenda watu huko, lakini hakika si ule moshi-moshi walio nao huko chini kwenye bonde hilo.

4 Nilizaliwa huku nje kwenye moja ya safu hizi huku Kentucky, nami siwezi kabisa kuiepuka, mwajua. Ninaninii tu, mimi . . . Hiyo ni . . . Huenda ikawa, kila mtu anaweza kukimbilia huko nje wakitaka, lakini kwangu mimi, afadhali nikae tu huku juu ambako unaweza angalau kupumua, macho yangu yalichoma, koo langu likawa jekundu.

5 Nami—nami nawaambia, ninaamini kwa njia fulani dhambi husafiri, vema, daima husafiri, nayo imesafiri pamoja na ustaarabu, dhambi daima huja kwa ustaarabu. Kabla hapajakuwapo na yeyote wa wazungu huku magharibi, wakati ilikuwa ni Wahindi watupu, hawakuwa na dhambi, waliishi tu maisha mazuri ya utulivu, nao walikuwa na shida ndogo ndogo, mara kwa mara, za vita vyao vya kikabila, na kadhalika, lakini ku—kuhusu *dhambi*, ilikuja na jamii ya wazungu, wakati ustaarabu ulipokuja. Walikuja pamoja na wanawake, wiski, na kucheza kamari, na mauaji.

6 Na kama vile jua lilivyoenda kutoka mashariki hadi magharibi, ustaarabu unasafiri pamoja nalo, nami ninaamini Bwana lazima ana skrini kubwa ya rada huku Pwani ya Magharibi, kwa sababu kama likiendelea mbele zaidi, litarudi mashariki tena, kwa hiyo nafikiri linatua tu dhidi yake, kisha linarudi moja kwa moja nyuma, kama wimbi. Nami ninasema ya kwamba hakika ndivyo ilivyo, bila shaka tunaishi katika wakati wa kutisha, wakati wa kutisha. Sasa, hilo halihusu tu Pwani ya Magharibi, na mimi kujivunia hawa Wabukeye, na Wahoosia, na

watafuna mahindi hapa, bali tunayo huku juu, pia, mwajua, bali ni zaidi yake tu huko nje.

7 Siku hizi tano usiku tulizo nazo, sasa hivi tulizo nazo, hapa Ohio tena. . . Nafikiri kesho usiku wanaenda kwenye jumba fulani la mikutano, ama kitu fulani, bali ni—nilifurahi kuja kanisani, napenda kanisa. Naam. Na—nafikiri kwamba, Ndugu Sullivan, katika—katika tu—tukio la usafiri, kwa kuwa ninaona ya kwamba mikutano iliyo bora zaidi daima ni makanisani.

8 Sasa, nina. . . natumaini mimi si mshirikina, kama ndivyo nilivyo sijui, lakini basi, unapoingia mahali hapa ambapo wana burudani, na kucheza kamari, na madansi, basi inaonekana kwangu kana kwamba kuna pepo wadogo wameketi kila mahali, mwajua. Nao kwa namna fulani ni ma—makazi yao, wanakaa tu pale, halafu inakubidi kuingia, inachukua kama siku tano usiku kuwahubiri wote wakatoka, mwajua, kabla hujaweza kuanzisha mkutano.

9 Lakini katika nyumba ya kanisa ninaamini Malaika wa Mungu hufanya kituo kuzunguka, kwa sababu watakatifu wakikusanyika pale, ni mahali maarufu pa Mungu, ambapo Yeye huja na kukutana na watu Wake. Sikuzote limeonekana ni jambo zuri kwangu kuwa kanisani. Ninalipenda zaidi, ili uweze kuwa, inaonekana kana kwamba ni nyumbani, mwajua, ni—ni mahali ambapo tunashiriki tu pamoja, na kuwa na mambo shirika.

Wakati Ndugu Sullivan, nasi tulipata nafasi ya kurudi tena, bila shaka nilifurahi.

10 Nimekuwa tu kwa majirani, huku Virginia, juma lililopita, na huko chini Richmond, tulikuwa na wakati mzuri sana huko chini pamoja na hao watu wa kusini. Wanapaita, "Mahali pa kuzaliwa kwa taifa." Nao wote ni watu wazuri wa kusini, pia, kweli wanampenda Bwana huko chini, nasi tulikuwa na wakati mzuri sana. Lakini nilikuwa na shauku ya kurudi nyumbani tena, hapa juu, ili tuweze kuabudu pamoja kwa muda kidogo.

11 Sasa, nina furaha kuwaona marafiki zangu hapa kutoka kaskazini. Uko umbali gani kutoka hapa, Charlie? Unaishi umbali gani huko. . .? [Ndugu huyo anasema, "Maili sabini."—Mh.] Yapata maili sabini. Vema. . . ["Upande huu tu mpakani mwa wa jimbo la Indiana."] Ndani tu ya mpaka wa jimbo la Indiana. Rodney na wote. . . ["Upande *huu*."] Ni kitu gani hicho? Upande huu? Upande huu wa mpaka wa jimbo la Indiana. *Karibu* tu aingie katika neema, bali aliikosa tu kidogo, kidogo tu, mpakani tu mwa jimbo.

12 Sasa, kama ungeshuka uje Kentucky, ungekuwa sawa kabisa. Ni Wakentaki wangapi walioko hapa ndani? Loo, jamani! [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Nawaambia! Kuna. . . Nilisema wakati mmoja kwenye. . . [Ndugu Sullivan anazungumza na Ndugu Branham.] Ati

msamaha? [Ndugu Sullivan anasema, "Unafikiri wangekuwa wakifanya nini nami . . .?. . . "] Sijui kabisa, Ndugu Sullivan.

13 Mama yangu alikuwa akihudumia nyumba ya wageni huko Jeffersonville, nami nina maskani yenye ukubwa kama huu, nadhani, kule. Usiku mmoja nilikuwa nikihubiri, nikasema, "Wote kutoka Kentucky simameni." Hakuna mtu aliyeketi chini, kila mtu . . . Nami nikasema, "Vema, Wakentaki, na panyabuku waliiteka hii nchi pasipo kufyatua risasi." Nikasema, "Wa—wao kweli waliingia mumu humu, wakaja moja kwa moja na kuinyakua. Vema," nikasema, "iliwabidi kutuma baadhi ya wamishenari hapa kutoka mahali fulani kusudi, ni ninii nzuri . . . kutoka . . . " Sizungumzi kuhusu Ohio sasa. Sasa, ngoja kidogo, ninazungumza kuhusu Indiana, huko chini Indiana.

14 Vema, popote uendapo, kote ulimwenguni, unakuta kwamba watu wa Mungu daima wako sawa. Niliona huko chini Afrika, na nchi zingine ambako nimekuwa, baadhi ya watu hao hata wasingeweza kujua mkono wa kulia na wa kushoto ni upi, lakini mnajua kinachotukia wanapompokea Roho Mtakatifu, yale wanayofanya? Jambo lile lile mfanyalo ninyi mnapompokea Roho Mtakatifu, wanatenda vivyo hivyo. Nao wata—watanena kwa lugha.

15 Nao, ungewazia kama walikuwa wakinena wenyewe, wakati mngesikia lugha yao, kama labda, kuna aina moja kule ambayo sikuzote ilinishangaza, kwa njia fulani wao hualika ndimi zao wanapozungumza, ninaamini wanaitwa Wabasuto, nafikiri ndivyo, la, Wakhosa. Na ukisema tu "Khosa," si sahihi. Inakubidi kualika, *Khosa*, kama *Khosa*. Na kila kitu unachosema kina mwaliko kwake, lakini wanapoanza kunena kwa lugha, wakati mwingine wazungumza Kiingereza. Mnaona? Na ninii tu, ninyi . . . wakati tu hao watu katika nchi hizo za makafiri wanapompokea Roho Mtakatifu, wanatenda tu kama mtu mwingine yeyote, haidhuru ni wapi, wao . . . Inaonyesha ni kwa "yeyote atakaye, na aje."

16 Sasa, nanii zetu, wengi wa ndugu zetu sasa wamesimama, na—nami kwa namna fulani nina ninii . . . nasikitika, laiti ningaliweza kuwapa mahali pa kuketi, lakini hatuna kabisa. Kwa hiyo nitaninii, sitazungumza zaidi ya saa tatu, ama kitu kama hicho, nadhani. Nami nilikuwa nikitania tu. Lakini upesi tu tuwezavyo kuwa na . . . kusikia Bwana akitubariki, na kusema imetosha, vema basi, tutataka kuninii, tutafumukana. Lakini kuwa na wakati huu wa ushirika hapa, jamaa hajui mahali pa kuanzia, ni ajabu sana na ni sawa.

17 Tumekuwa na mikutano mikubwa kwenye Pwani ya Magharibi, kama nilivyokuwa nikisema. Bwana kweli alibariki sana huko Pwani ya Magharibi wakati huu, nilienda karibu na Visalia, huko juu, na huko ni Bakersfield, na Fresno, na kupitia kule, walikuwa watu wenye mioyo iliyo na njaa kwelikweli huko

chini kupitia kwenye hayo mabonde. Ninaamini sababu ya mi—mimi kuwa na njaa, ni kwa sababu Mungu analiita Kanisa Lake pamoja, likila Neno la Mungu.

18 Sasa, kabla hatujaanza, tunapaswa kuzungumza na Mwandishi, nafikiri, kabla hatujasoma Neno Lake. Hivi hamwoni hivyo? Kwa hiyo na tuinamishe vichwa vyetu sasa, na kuweka kando mambo yetu yote ya kitoto, na kuangalia sehemu iliyo kali sana, na takatifu, Neno.

19 Baba yetu wa Mbinguni, tunapokusanyika hapa, usiku wa leo, katika kanisa hili, kanisa linaloitwa kwa Jina Lako, watu waliokusanyika hapa wanaitwa kwa Jina Lako. Nawe ulitupa ahadi katika Neno Lako la Milele, "Ikiwa watu wanaoitwa kwa Jina Langu watakusanyika pamoja na kuomba, basi nitasikia kutoka Mbinguni." Sasa, hiyo ni ahadi Yako, nasi tunajua ya kwamba Wewe hutimiza ahadi Zako zote kwa watu Wako. Tunakushukuru kwa ajili ya kanisa, na kwa kila mtu ambaye amewakilishwa hapa, na kila kanisa ambalo limewakilishwa. Nasi tunaomba, Bwana, ya kwamba utatubariki pamoja kama watoto Wako waaminio.

20 Usiku wa leo, tungeomba, hasa, kwa ajili ya Ndugu yetu mwema na mwaminifu, Sullivan, kwamba ungembariki sana, kwa wingi, kwa kuwa shauku ya moyo wake ni kukutumikia Wewe, na kukufanyia jambo fulani, na kufanya saa zake zote kuwa na faida kwa ajili ya Ufalme, akiwaleta wahudumu mjini, wahudumu mbalimbali wenye aina mbalimbali za huduma, wapate kutumikia kusudi, na apate kulisha kundi ambalo Roho Mtakatifu amemweka kuwa mwangalizi wake. Tunakushukuru kwa ajili ya jambo hili.

21 Na kwa kuwa ni chaguo letu sasa, kama ni mapenzi Yako kulilisha kundi hili kwa siku nne au tano zijazo hapa, tunaomba ya kwamba Roho Mtakatifu atawapa Chakula cha ko—kondoo, Neno, alilete kwa nguvu na madhihirisho ya Roho Mtakatifu. Tubariki tunapokungojea Wewe. Waokoe wale wote wanaoweza kuokoka, Bwana, mjaze mwaminio anayengojea kwa subira kumpokea Roho Mtakatifu, tunaomba ya kwamba utamruhusu kila mmoja aliye katika hali hiyo aondoke hapa usiku wa leo, mwenye furaha, ameokoka na kujazwa na Roho pia.

22 Waponye wagonjwa, Bwana. Wewe umetupa agizo, "Nendeni mjini, waponyeni wagonjwa walioko . . . mji huo, ama, mkahubiri ya kwamba Ufalme umekaribia." Mungu tunaomba ya kwamba utatujalia mambo haya kama watumishi Wako, kama mabalozi Wako, kwa sababu tunaamini ya kwamba Ufalme umekaribia. Na utusaidie kulileta Neno hilo kwa njia hiyo, ili watu wapate kuona, na kukuamini Wewe. Na kwenye ile Siku kuu ya kutoa hesabu inayowajia wote, jalia, kwa sababu ya jitihada zetu, kutakuwako na mamia watakaosimama pale, waliokombolewa kwa Damu, kwa sababu ya jitihada tunazojaribu kutoa sasa.

23 Baba, tunapokuja pamoja, tunazungumza kama watoto, tuna furaha. Na sasa tunaomba ya kwamba Wewe utatujalia kuweka kando hayo, na kuingia katika kazi ya Ufalme, na kuwa chini ya Roho Mtakatifu. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu, na kwa ajili Yake. Amina.

24 Sasa, kwa njia ya muktadha mdogo, huenda nikawaelekeza kwa Wakorintho wa Kwanza, mlango wa 14, na kifungu cha 8:

> *Maana baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, ni nani atakayejifanya tayari* kwa *vita?*

25 Tunaishi katika wakati wa mashaka. Karibu kila kitu tunachoangalia siku hizi kina mashaka. Tunaishi katika wakati ambapo, inaonekana, ni vigumu kwako kuweka mkono wako juu ya kitu chochote kilicho hakika. Usalama wetu wa taifa, hauna uhakika kabisa, tunaona kwamba katika hilo, sababu ya sisi . . . wote, nasema usalama wa kimataifa, kwa sababu kwamba tuko tu katika mwisho wa wakati.

26 Siku chache zilizopita huko California kulikuwako na u—ujumbe uliotolewa wakati ndugu Mbaptisti alipokuja kutoa, ama, kunipa mkono, baada ya mkutano wa Wafanyabiashara kwenye—kwenye kiamshakinywa cha Mkahawa wa Clifton. Ni ndugu yake Marilyn Monroe, nafikiri ndiye, yule mchezaji maarufu wa sinema. Yeye ni Mbaptisti, naye akaanza kunipa mkono, alipofanya hivyo akaanza kunena kwa lugha zisizojulikana. Basi ikatokea kwamba kulikuwako, mwanamke kutoka Louisiana, naye alielewa Kifaransa, naye akasema, "Huyo mvulana alizungumza Kifaransa."

Akasema, "Sijui hata neno moja la Kifaransa."

27 Ndipo wakati alipotoa tafsiri ya yale aliyosema, mkalimani wa UN alikuwapo, naye akamjia huyo mama, na kwa Wa—Wafanyabiashara, na kusema, "Huyu mama alifasiri vizuri kabisa." Kasema yeye hufasiri katika UN. Akinipa ujumbe.

28 Halafu basi, ninaamini ilikuwa ni seneta wa jimbo fulani alikuwa tu akizungumza na Ndugu Shakarian, na huko juu Greenland ambako taifa hili limejiandaa kutoka Greenland kuiangamiza dunia kwa silaha za atomiki, mguso mmoja tu na taifa lolote litaondolewa moja kwa moja duniani. Mnaona, jambo pekee tunalosikia ni ninii tu, "Wana bomu litakalofanya mambo *fulani-fulani*," bali wana kubwa kuliko hizo, mwajua. Hawaninii . . . Hutoi ninii zako, siri zako zote zikiwa zinazohusu mambo ya kitaifa.

29 Basi mtu huyu anakuja Miami Julai, ambako nitafanya mkutano huko Miami, Florida. Na kulikuwa na ko—kombora lililoingia kwenye skrini nao, kitu fulani kwenye skrini, naye mtu huyu alikuwa na amri ya kuvuta wenzo, na hiyo ingekuwa *ndiyo*. Lakini alisema mwenyewe kwamba asingeweza kuivuta, ambayo ingeachilia, sijui ni makombora mangapi makubwa ya mabomu na chochote kile, ndipo vita vingekuwa vimeanza. Lakini *kitu*

*fulani* kisingemruhusu kuivuta. Sijui kama huyo alikuwa ni Mungu, kwa kuwa kuna mtu hapa ambaye bado hajaokoka, kwamba kamwe haliwezi kutukia mpaka jambo hilo litukie. Hiyo inaonyesha tu jinsi tulivyo karibu.

30 Mnaona, yule Malaika alimwambia Lutu, "Toka hapa, kwa sababu siwezi kufanya lolote, hata utakapokuja huku." Hana budi kuondoka kwanza, kabla hajaweza kufanya lolote kulihusu.

31 Kwa hiyo miaka mingi iliyopita, mataifa makubwa ndiyo yaliyokuwa na nguvu, yale yaliyokuwa na meli kubwa kubwa na watu wengi, kama vile Uchina, na Urusi, na Marekani, yalikuwa ndiyo mataifa yenye nguvu, hilo halipo tena, taifa lolote dogo linaweza tu kuiangamiza dunia nzima. Kwa hiyo, sio ukubwa wake tena, ni kungojea tu wakati.

32 Sasa, hebu tusiangalie hilo kijuujuu sana. "Loo," unasema, "Ndugu Branham, nime—nimesikia mambo kama hayo hapo awali." Ninajua hilo, bali mtalisikia wakati mmoja, kwa mara ya mwisho. Na mengine yote yamekaribia sana, nitayasikia karibu wakati wowote. Basi tunapaswa kuwa watu wa aina gani wakati huu? Mwenye dhambi anapaswa kuwa anapiga mayowe apate rehema, naye Mkristo anapaswa kuwa akipiga makelele ya kumsifu Mungu. Sawa.

33 Mtu fulani alisema wakati mmoja, kasema, "Ndugu Branham, unawatisha watu kwa kusema Yesu yuaja upesi sana. Mbona, ni jambo la kuchukiza sana kuwazia ya kwamba ulimwengu wetu unafikia mwisho!"

34 Nikasema, "Si kwa Mkristo, ndilo jambo tukufu sana awezalo kuwa nalo niani mwake, kuwazia tu ya kwamba Bwana wetu anaweza kuja wakati wowote. Yote yatabadilishwa wakati huo, yatakwisha."

35 Ninaamini hao wavulana wana kitabu kidogo hapa ambacho Wafanyabiashara walikichapisha, ono ambalo Bwana alinipa hivi majuzi. Natumaini mtakisoma.

36 Naam, Paulo alisema, "Nimevipiga vita vilivyo vizuri, na mwendo nimeumaliza, na imani nimeilinda. Tangu sasa nimewekewa taji ya haki, Bwana, Hakimu mwenye haki, atanipa Siku ile, wala si mimi tu, bali na wote *wanaopenda* kuonekana Kwake." Loo, unapompenda Bwana, inaondoa hofu yote. Unaenda tu kumlaki Yeye.

37 Hivi majuzi, wakati rafiki yangu wa zamani, Dk. F. F. Bosworth, alipokufa huko Miami, nilishuka kwenda kumwona. Alikuwa na umri wa karibu, karibu sana miaka tisini. Ndipo nikamwambia, nikasema, "Ndugu Bosworth, wakati wa furaha sana maishani mwako ulikuwa ni upi? Umekuwa ukihubiri sasa kwa yapata miaka hamsini na mitano au sitini."

Akasema, "Hii ndiyo saa ya furaha sana niliyopata kuishi."

Nami nikasema, "Ungeninii...? Kwa nini useme hivyo?" Nikimhoji tu huyo mzee mtakatifu.

38 Akasema, "Ndugu Branham, yote ambayo nimeishia tangu nilipokuwa kijana, imekuwa ni Yesu Kristo." Naye akasema, "Karibu dakika yoyote, ninamtazamia Yeye aingie mlangoni anichukue twende pamoja Naye." Kasema, "Ndio wenye furaha sana! Yote ningaliweza kuwazia, ama matarajio mazuri sana ambayo ningeweza kuwa nayo, ni kujua ya kwamba hivi karibuni sasa nitakuwa mikononi mwa Bwana wangu, nipate kuwa pamoja Naye milele." Huyo ni Mkristo halisi akifa, huyo si Mkristo halisi akifa, huyo ni Mkristo halisi akienda-kuwa-pamoja na Yeye.

39 Kama vile Paul Rader alivyosema, alipokuwa akifa, Los Angeles, kama tunavyoita mauti, alimwita ndugu yake, Luke, akasema, "Wazia jambo hilo, Luke, tumekuwa pamoja kwa muda mrefu, lakini," kasema, "katika dakika tano tangu sasa, nitakuwa nimesimama Mbele za Yesu Kristo, nimevikwa haki Yake." Akauminya mkono wa ndugu yake, akaenda kukutana na Yeye. Loo, hilo linanifanya niwazie *Zaburi Ya Maisha* ya Longfellow:

> Maisha ya watu mashuhuri yote yanatukumbusha
> Nasi tunaweza kuyafanya maisha yetu adhimu,
> Kwa kutengana, tunaacha nyuma yetu,
> Kumbukumbu za kudumu.

Jinsi hilo linavyomtia moyo Mkristo!

40 Nilikuwa na kitabu, nadhani ninacho mahali fulani nyumbani, ya watu mashuhuri, maneno ya mwisho kabla hawajaondoka ulimwenguni, mwenye dhambi na mtakatifu pia. Nina akina Dwight Moody, na wengi wa watakatifu wengine mashuhuri waliouacha ulimwengu. Moody, wakati mauti yalipompiga, yeye alisema, "Ati mnaita hiki mauti?" Akasema, "Hii ndiyo siku ya kutawazwa kwangu."

41 Nao malkia, malkia mmoja wa Uingereza, mwovu sana, alisema ya kwamba angeutoa ufalme wake apate kuishi dakika kumi na tano zaidi. Mnaona, mwishoni mwa safari inasimuliwa. Na hapo ndipo tulipo, mwishoni mwa safari.

42 Hakuna uhakika katika usalama wa taifa tena, kwa sababu huwezi kuchimba vya kutosha chini ya ardhi, kuwazuia wasikulipulie mbali, huwezi, hakuna la kufanya, tuko tu kwenye mwisho wa safari. Nasi tunachukua basi, na baadhi ya mambo mengine, hakuna uhakika.

43 Nilikuwa nikisikiliza matangazo ya habari nikija huku, kwamba kuna watu wengi zaidi wasio na kazi sasa, kuliko ilivyokuwa wakati ule wa—wa enzi za Rais Hoover za kuzorota kwa uchumi, watu wengi wasio na kazi kuliko ilivyokuwa wakati wa utawala wake, na katika wakati wa 1930, mahali fulani hapo.

44 Wengi wetu wa wakati huo, tunakumbuka jambo hilo, wakati tungekula kidogo, viazi vichache vyenye wadudu wadogo juu yake, na kuwala hao wadudu na kadhalika, kwa sababu tulivipata tu mara kwa mara, na kuvila kwenye kiamshakinywa, chakula cha kutwa, na chakula cha jioni. Jinsi ilivyokuwa ngumu! Na sasa, kwa sababu wanaweza kusema ya kwamba, kuna karibu theluthi moja zaidi ya watu Marekani, kuliko ilivyokuwa wakati huo.

45 Na hivi majuzi, nikija Richmond, Louisville, na mahali pengi, mnajua jinsi ninavyowazia baadhi ya viongozi wetu ndio wanaoleta hili, kuona kwenye kona ya barabara, polisi wanawake. Mwanamke ana shughuli gani, kuwa polisi, kupambana na walevi, na kadhalika, huko nje? Hiyo inapaswa kuwa ni kazi ya mwanamume. Kama wangewarudisha baadhi ya wanawake hawa jikoni ambapo ndipo mahali pao, wanaume wangekuwa na kazi nyingi zaidi, kungekuwa na nyingi zaidi. Lakini wao. . . Ni saa ile tu hata hivyo, ukosefu wa kazi, hakuna wakati, hakuna kitu kilichosalia, ni vigumu kuweko, ila kuja kwa Bwana, kurekebisha mambo yote. Ajira!

46 Maisha ya nyumbani hayana uhakika. Hatujawahi kuwa na wakati ambapo tulikuwa na talaka nyingi sana katika wakati wa amani, kama tulivyo nazo sasa. Maisha yetu ya nyumbani yamevunjika-vunjika. Miaka mingi iliyopita, ilikuwa kwamba—kwamba mama na baba walikuwa nyumbani usiku, kama si nyakati za kanisa, ama chochote kile. Nao kamwe hawakuwaacha watoto wao wazurure mitaani, na kukimbia huku na huku usiku kucha, na siku hizi inaonekana kama ndiyo maoni ya watu wengi.

47 Loo, jinsi unavyoenda tu kwenye nyumba ya kisasa siku hizi, unaangalia jinsi ilivyo, Baba, inambidi kuharakisha kwenda kwenye chumba cha kamari, nao wavulana wanacheza biliadi, ama wanachezea mpira, ama chochote kile, yeye na Ma; dada yuko kwenye kantini, mahali fulani, ama kwenye karamu ya roki; Kadogoo ana gari la kasi, huko nje akiona ni wangapi anaoweza kukanyaga, na hayo karibu ndiyo maisha ya nyumbani. Nayo Biblia? Loo, ni Kitabu kikuu, bali kimewekwa kwenye mtoto wa meza mahali fulani, mpaka Mchungaji atakapoingia, ama mtu fulani. Nasi kamwe hatuna maisha ya nyumbani tuliyokuwa nayo. Ni ninii. . . Maisha ya nyumbani hayana uhakika kabisa.

48 Mwanamume, siku hizi, anapooa, nyinyi vijana, afadhali mwombe muda mrefu, mwombe Mungu akupe mwenzio, ninyi wasichana, vivyo hivyo, maana hayana uhakika *kabisa*. California, ninaona huko, ya kwamba na—nafikiri ilikuwa ama asilimia kumi na tano, ama ishirini, kitu kama hicho, cha upotovu, watu waliopotoka wameongezeka katika mwaka mmoja ama miwili iliyopita. Loo, ni—ni mbaya sana! Na maisha ya nyumbani hayana uhakika.

49 Siasa, hazina uhakika, hakuna uhakika katika siasa tena. Vyama hata haviwezi kuwa na uhakika wowote; hakuna haki yoyote miongoni mwao tena. Sasa, mtu anaweza akasema, “Hupaswi kutaja siasa mimbarani.” Hiyo ni kweli. Lakini uadilifu na Ukristo vinapaswa kutajwa mimbarani. Hiyo ni kweli. Mimi, si mwanasiasa, mimi ni Mkristo. Pande zote mbili zimepotoka.

50 Lakini hivi majuzi tu, katika uchaguzi wa Rais, hata iliwabidi kurudi na kuona mitambo hii ya kupigia kura, kwamba wakati ungeninii. . . waliikarabati ili kwamba unapompigia mmoja kura, i—ingekubidi kumpigia kura huyo mwingine pia, upotovu. Haijulikani ni nani aliyechaguliwa, hawawezi kujua tena, hakuna uhakika humo. Unawaketisha chini kuhesabu kura, ndipo mtu fulani ni mpotovu vya kutosha kuzihesabu kwa njia mbaya. Vyama, viking’ang’ania kumwingiza mtu wao, hakuna uaminifu.

51 Sasa, kama Bw. Kennedy angalikuwa ni Mrepablikani, ama—ama chochote kile, Mdemokrati, Bw. Nixon, haikuleta tofauti yoyote, hilo ni jambo baya wakati mitambo inapovurugwa ipate kudanganyia kura. Nao FBI wakathibitisha ya kwamba jambo hilo lilitendeka, bali hawakufanya lolote kulihusu. Mnaona? Kwa nini? Unashangaa ni kwa nini mambo kama hayo yanapita juu ya uso wa watu, jinsi yanavyotukia kamwe. Ni kwa sababu mambo haya hayana budi kuwa, tuko katika wakati wa mwisho, hayana budi kuwapo, ilibidi mtu huyu achaguliwe, tuko mwisho. Nami nina hakika ya kwamba mnaweza kufanya mbili na mbili kuwa nne, kwamba tuko kwenye wakati wa mwisho. Nayo mitambo hii, haidhuru wangeweza kuthibitisha kiasi gani kwamba *waliivuruga*, haina budi kubaki jinsi ilivyo.

52 Ndipo mtu fulani akaniambia, mhudumu mmoja akanipigia simu, mmoja wa wadhamini wa mkutano uliofuata, mmoja wa mikutano iliyofuata nchini, kasema, “Ninasikia kwamba wewe, unahubiri sana dhidi ya akina dada kanisani mwetu kukata nywele zao, na—na kuvaa kaptura, na kadhalika.”

Nikasema, “Naam.” Nikasema, “Sasa, ka—kama hutaki kusikiliza hayo, basi usiagizie niitwe.” Mnaona?

Naye akasema, “Unafikiri utawahi kulikomesha?”

Nikasema, “La. Wewe unaamini kamwe utawahi kuikomesha dhambi?”

Akasema, “La.”

53 Nikasema, “Vema, kwa nini unahubiri dhidi yake basi?” Mnaona? Kosa, ni kosa, mtu fulani hana budi kulikemea. Kweli. Sema kweli, kwa maana ghadhabu ya Mungu itakapomwagwa, basi hutaninii. . . hutakuwa na udhuru.

Naam, kisiasa, siasa, kazi, usalama wa taifa, kila kitu hakina uhakika.

54 Sasa, tunashuka kuja kanisani. Kanisa, *linavyojiita*, halina uhakika. Sasa, tuna yapata madhehebu mia tisa mbalimbali humu, Marekani hii, sasa, na kila moja linalipinga lingine, kwa hiyo ni wapi mnajua kile. . . unajuaje la kufanya juu yake? Unaninii tu. . . Ni wakati wa mwisho tu, tuko kwenye mwisho wa safari.

55 Na kadiri ninavyoyaheshimu hayo, kila moja la hayo, afadhali niwe na Mmethodisti *hapa*, Mbaptisti *pale*, Mpresbiteri *hapa*, na kadhalika, na kuwa nao kote nchini, kuliko kuwa na baa, na vilabu vya pombe haramu, na kadhalika, watafaa kidogo, haidhuru wako wapi, kama ni misheni ndogo, na—na . . . Kama vile mtu fulani alivyosema, nami natumaini siudhi hisia za mtu yeyote, wakati mtu fulani aliposema, "Afadhali niwe M—Mkampbeli kuliko kutokuwa na *Nuru* hata kidogo." Kwa hiyo, nadhani hiyo karibu ni sawa. Sasa, haidhuru ni nini, watafaa ki—kidogo, nasi tunawahitaji wote.

56 Lakini huo haukuwa ndio mpango wa Mungu, huo ulikuwa mpango wetu, kuyaunda makanisa yetu na madhehebu, tulilijaribu hilo katika bustani ya Edeni, ni ya kale kama Edeni ilivyokuwa. *Dini* maana yake ni "kifuniko." Naye Adamu alijaribu kujifunika apate kujitengenezea njia yake mwenyewe, akajifunika, lakini haikufanikiwa.

57 Kuna mahali pamoja tu ambapo Mungu hukutana na mwanadamu, hapo si katika elimu yake, si katika dhehebu lake, ushirika wake, ni chini ya damu. Na hapo ndipo mahali pekee ambapo Mungu aliwahi kufanya, ama atakapokutana na mwanadamu, ni chini ya damu, hapo ndipo mahali. Mungu aliweka mpango katika bustani ya Edeni kwa damu iliyomwagika.

58 Na kama Mungu akiwahi kufanya uamuzi, Yeye hawezi kuubadilisha, kwa sababu Yeye ni mkamilifu, basi kila kitu anachofanya na kusema ni kikamilifu. Kwa hiyo Yeye hawezi kubadilisha mpango Wake almuradi kuna ulimwengu na almuradi kuna mwenye dhambi, kuna njia moja tu, tangu bustani ya Edeni, wakati dhambi ilipofanywa kwanza, mpaka dhambi ya mwisho itakapofanywa, kuna mpango mmoja tu wa ukombozi, huo ni kupitia kwa damu iliyomwagika, hakuna kitu kingine kitakachofanya kazi, kanuni zetu za imani, madhehebu yetu, na kila kitu kimetekeleza sehemu, na sehemu nzuri, bali si mpango wa Mungu, mpango Wake ni kurudi kwenye ile damu.

59 Kwa hiyo makanisa pia yana sauti zisizojulikana, moja ya hizo inasema, "Siku za miujiza zimepita." Hilo halijulikani kabisa kwa Biblia. Mnaona? Hilo lingine linasema, mbona, mambo mbalimbali na, "Huna budi kukariri kanuni *hii* ya imani, kisha huna budi kufanya *hivi*, na *vile*," na kadhalika.

Vema, kutokuwa na uhakika sana, kwa sababu kuna mengi mno, yanafanya kila namna ya—ya—ya mambo mbalimbali kupingana, moja likipinga *hili* na kupinga *lile*, na yapata asilimia tisini na tano yake ni kinyume na Biblia.

60 Kwa hiyo, kuna sauti isiyojulikana miongoni mwa makanisa, miongoni mwa siasa, miongoni mwa nyumbani; kila kitu kinaonekana kutokuwa na uhakika.

61 Sasa, Biblia ilisema, hapa, katika Timotheo wa Pili 3:7, ya kwamba siku hizi zitakuja, ilisema ya kwamba wangekuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu. Sasa, hiyo ni kweli. Televisheni imekuja nyumbani na kuwazuia watu wasiende kwenye mikutano ya maombi, ina mvuto wake ambao ni wa kuvutia na unapendeza.

62 Nami sisemi ya kwamba baadhi ya vipindi vyake si sawa, kuna vingi vyake ambavyo si sawa, tunajua hivyo. Lakini sininii. . .Naam, asilimia tisini na tisa yake si sawa, lakini tuseme kungekuwa na asilimia moja yake. Vema, unachopata katika hiyo asilimia moja, hivi ungekusudia kutoa asilimia hiyo moja kwa ajili ya Kanisa la Mungu aliye hai, ambapo hilo ni sawa asilimia mia moja, usihudhurie mikutano ya maombi Jumatano usiku?

63 Lakini dhambi inavutia, vyovyote unavyoichukua, dhambi inamvutia mwanadamu, kwa sababu yeye ni raia wa—wa jamii iliyoanguka tuliyo sisi. Nayo inavutia, Shetani anajua jinsi ya kuifanya ivutie, yeye ni—yeye ni hodari kazini mwake. Naye, na kama hawezi kuipeleka huko nje katika mambo ya ulimwengu, anaileta moja kwa moja kanisani, anakuja moja kwa moja kwenye uwanja wetu wenyewe. Hiyo ndiyo sababu, ndugu, dada, tunapaswa kumtambua. Wakati umewadia ambapo Kanisa lilikuwa la kiroho kumtambua, kumjua Mungu, si kwa kanuni za imani, si kwa madhehebu, bali kwa tukio, kujazwa na Roho Mtakatifu.

64 Siku chache zilizopita, huko California, ndiyo kwanza nitoke Beaumont, mahali mbalimbali, ambako tumekuwa tukifanya mikutano, nao upako wa Roho Mtakatifu ulikuwa mkubwa juu yangu wakati huo, kama unavyokuwa kwako, na sisi wengine, nawe ungeweza kutembea mtaani na kuhisi tu hiyo presha. Sasa, kama huna upako huo juu yako, huuzingatii sana, unaendelea mbele tu. Sikilizeni, enyi kanisa, hiyo ndiyo sababu mtu fulani anafikiri mimi ninawakemea sana, sivyo, sitaki kuwakemea watu. Lakini kama ukishuka tu chini ya upako, ambapo unaweza kuuhisi Uwepo wa Mungu, kisha uingie penye dhambi, inakugeuza, wala huwezi kunyamaza, huna budi kusema jambo fulani, na ni upako wa Roho Mtakatifu.

65 Ndipo unapowaambia watu, "Je, wewe ni Mkristo?" Vema, upesi watakwambia wao ni wafuasi wa dhehebu fulani,

ama shirika fulani, unaona, nao wa—wameridhika nalo. Wanaonekana kufikiri ya kwamba hayo tu ndiyo yanayotosha, hayo tu ndiyo hayana budi kuwa, kama wao ni wafuasi wa dhe—dhehebu fulani, hilo tu ndilo linalowabidi kufanya. Vema, hiyo ilikuwa kwamba tuliwaita hao watu Wabaptisti baridi, wa kawaida, na Wamethodisti, lakini sasa ni Wapentekoste baridi, wa kawaida, wameenda hivyo pia. Ni—ni katika kanisa la Kipentekoste, kila mmoja anataka kusema, "Mimi ni mfuasi wa *hili*," ama, "Mimi . . . " na hilo ni sawa, sihukumu hilo, hilo ni sawa. Lakini kile unachotaka kuwa, kama ukikiri Pentekoste, Pentekoste ni tukio ambapo mwanamume au mwanamke, mvulana au msichana huzaliwa mara ya pili kwa tukio la Kipentekoste la Roho Mtakatifu.

66 Na mara unapompokea huyo ulimwengu wote unaonekana kukulemea. Loo, umejifunga nira pamoja na Kristo. Nalo lilileta machozi machoni Mwake, na huzuni, hata mauti kwa mwili Wake, wakati ulimwengu katika siku *hiyo* ulikuwa wenye dhambi sana. Unafikiri inafanya nini siku hizi?

67 Nilikuwa mahali fulani, ninaamini ilikuwa ni huko Athene, ama mahali fulani, nami ni—nikaona pi—picha, kama sahani, ukutani. La, sa—samahani, ninayo kwe—kwenye santuri ama ile sinema maarufu ya *Dakika Tatu Ifike Usiku Wa Manane,* ambapo sayansi inasema hapo ndipo tunapoishi, dakika tatu kufikia usiku wa manane, na hilo lilisemwa yapata miaka mitatu, minne, au mitano iliyopita, ninaamini tuko katika sekunde sasa, za kusogea kwa wakati. Sasa, ninaweza kuwa nimekosea, lakini inaonekana tu hivyo kwangu. Nao walikuwa na picha kama ya Kristo, kwenye sahani, na matone ya machozi, alipokuwa akiangalia chini duniani, yalikuwa yanadondoka kutoka usoni Mwake.

68 Sijui kama si kama tu ilivyokuwa katika siku za Nuhu, wakati Mungu aliposema hata ilimhuzunisha moyo kwamba Yeye alimfanya mwanadamu. Sijui kama halijafikia mahali hapo tena usiku wa leo, kwamba mtu yeye yule aliyemwumba, na kujitoa Mwenyewe kwa ajili yake, na kumkomboa huyo . . . kumkomboa mtu huyo, naye anamkataa tena usoni Pake.

69 Wakati huu wa kutisha tunaoishi, wa kujiunga tu na kanisa, huo ni (Kama unafikiri ya kwamba wewe ni Mkristo, na kitu fulani kikakwambia, ulikuwa Mkristo kwa sababu ulikiri, na kujiunga na kanisa, hiyo ni sauti isiyojulikana.), hiyo ndiyo sababu siku hizi, watu hawavutiwi na uamsho, hiyo ndiyo sababu ulimwengu hauutaki. Hatuna budi kuwa na sauti ya hakika kwake, sauti ya hakika.

70 Na sababu, siku hizi, kwamba tunapokuwa na mkutano mrefu, ama kukusanyika pamoja, hawapati sauti ya hakika. Lakini walipokuwa na uamsho kwenye Siku ya Pentekoste, kulikuja sauti ya hakika kutoka Mbinguni, kama upepo

wa nguvu ukienda kasi ulioijaza nyumba yote walimokuwa wameketi, hiyo ilikuwa ni sauti inayojulikana, ilikuwa ni thi—thibitisho ya kwamba Mungu alikuwa katikati yao.

71 Kanisa siku hizi, ni kama tu lilivyokuwa katika—katika Edeni, mashariki mwa hilo lango, huyo hapo Kaini, alijenga ma—madhabahu, akaijenga pale, na kuisimamisha katika kumbukumbu ya Yehova. Yeye hakuwa kafiri, alitengeneza madhabahu na, katika ukumbusho wa Yehova, na kuweka dhabihu juu yake, kisha akajilaza madhabahuni, na kumwita Mungu. Naye Mungu akakataa wito wake, kwa sababu haukuwa na sauti ifaayo, hapakuwapo na kitu pale cha kupaza sauti, kilichokuwa kikifa, hakukuwako na kitu, hakuna mauti ya kumtuliza. Dhambi hiyo ilibidi ilipiwe na mauti, "Siku mtakayokula, siku hiyo mtakufa." Naye akaweka maua, na kuyarembesha, bali hakukuwa na kitu pale cha kusema kwamba kulikuwa na mauti.

Ndipo kutoka kwenye madhabahu ya Habili kikaja kilio cha mwana-kondoo, kulikuwa na kifo cha kulipia adhabu, damu ilikuwa ikimwagwa.

72 Na siku hizi, wakati Mungu, kama tu ilivyokuwa katika siku ile alipomwambia Kaini. Kaini alivunjika moyo, akasema, "Haya *hapa* yaliyo mema zaidi ninayoweza kufanya, unaweza kuichukua au kuiacha, ufanye lolote utakalo kuihusu, lakini hayo tu ndiyo ninayoweza kufanya kuihusu."

73 Hivyo ndivyo Wakristo wa kisasa wanavyoabudu leo, "Ninaenda kanisani, ninawasaidia wahubiri, ninalipa zaka zangu, ni—ni—ni . . . Kama wakiingia kwenye karamu ya kijamii, ni—ni—ninatekeleza wajibu wangu kwake, Na kama—kama wanahitaji sadaka ya kimishenari, ni—ninasaidia katika hiyo." Hilo ni zuri, bali hilo silo Mungu analohitaji, hana budi kusikia sauti ya mauti. Asifiwe Mungu!

74 Kile Mungu anachotaka siku hizi, ni *wewe* ufe, ufe kwa mambo ya ulimwengu, na kwa nafsi yako, kusikia mayowe, "Bwana, nichukue jinsi nilivyo!" Hicho ndicho Mungu anachotaka, anataka sauti ile ya mauti, mchacharisho ule wa mauti ya Adamu wa kale, anayekufa, ili aweze kuingia na kuchukua mahali Pake, na kuwatawala, na kuwa Bwana wenu. Loo, ni wakati wa jinsi gani tunaoishi!

75 Sasa, tunaona Mungu alimwambia Kaini, Yeye alisema, "Endelea ukaabudu kama ndugu yako, Habili, nawe utafanya vema. Endelea na ufanye jinsi anavyofanya, itakuwa sawa kwako." Lakini kama hakufanya hivyo, dhambi ilikuwa mlangoni, na ni jambo lile lile leo. Kwa hiyo, tunaona ya kwamba hakuna sauti ya hakika kwa kanisa, *linalojiita* Kanisa.

76 Sasa, kanisa, tunafanya kanisa siku hizi, linalojiita *Kanisa*, madhehebu, tunasema hilo ndilo Kanisa. "Uh, wewe ni wa kanisa gani?" Mbona kuna Kanisa moja tu, kuna moja tu. Kuna

madhehebu mengi, bali Kanisa moja, madhehebu mengi. Na kama vile nimeninii, ninataka kuliweka wazi, sina kitu dhidi yao, yametekeleza sehemu kubwa, lakini hilo silo bado, silo.

77 Mbili. . .*Kanisa* linamaanisha "walioitwa watoke, waliotengwa." Na watu wawili hawawezi kuishi ndani yako wakati ule ule, huna budi kufa kwa mambo ya ulimwengu upate kumtumikia Mungu. Huwezi kumpenda Mungu na mali kwa wakati ule ule. Na almuradi kuupenda ulimwengu kumo ndani ya moyo wa—wa—wa mwaminio, yeye huyasonga kabisa na kujinyima majaliwa ambayo Mungu amempa. Mungu hataki upungukiwe, anataka uwe na kila majaliwa aliyokufia, kila majaliwa aliyolipa Kanisa, anataka uyafurahie, ni yako.

78 Vipi kama nilimnunulia mvulana wangu mdogo baiskeli, ama, naye angenirushia usoni mwangu, na kusema, "Sitaki kitu hicho"? Kutothaminiwa. Vipi kama ulimnunulia msichana wako mdogo mwa—mwanaserere mdogo, naye akamchukua na kukurushia tena? Hana shukrani. Mnaona, hivyo ndivyo tulivyo, tunapojaribu kuishi chini ya majaliwa ambayo Mungu alitupa. Kristo alikufa ili tupate majaliwa haya. Loo, jinsi ambavyo hana budi kujisikia leo wakati tumechukua mpango mwingine, na kumrushia Roho Mtakatifu usoni Mwake, na kusema, "Hatuhitaji ulokole huo tena, nitajiunga tu na kanisa. Mi—mimi ni. . .!"

79 Huwezi kujiunga na Kanisa, hakuna kitu kama kujiunga na Kanisa. Hu—huenda ukajiunga na madhehebu, bali huwezi kujiunga na Kanisa, kwa sababu huna budi kuzaliwa Kanisani, Huwezi kujiunga Nalo, huna budi kuzaliwa ndani Yake. Nao waaminio wote wanazaliwa katika Kanisa la Mungu, Kanisa la, si Church of God ya kimadhehebu, bali Kanisa la Mungu aliye hai, ambalo ni Kristo aliyefufuka katika wafu, na anayeishi miongoni mwetu. Hiyo ni. . .

80 Sasa, halafu kuna sauti zisizojulikana wanaposema, "Mimi ni wa Pentekostal Assemblies. Mimi ni wa Pentekostal United. Mimi ni wa Pentekostal Church of God. Mimi ni wa Pentekostal Holiness. Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mbaptisti. Mimi ni Mpresbiteri." Mambo hayo yote, yote ni sawa, kadiri hayo yaendavyo.

81 Simaanishi kukufuru kwa kusema jambo hili, maskini jamaa huyo mweusi, akila tikitimaji, walimpa kipande chake, wakakiandaa vizuri, naye akala, nacho kikatelemka tu chini namna *hiyo*, na kuzitema mbegu kutoka pembeni mwa kinywa chake, kasema, "Umeionaje Mose?"

82 Akaangalia ile sehemu nyingine yake kubwa, mwajua, ambapo hicho kipande kimoja kidogo kilitolewa, akasema, "Bosi, ilikuwa nzuri, lakini kuna zaidi." Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo, madhehebu haya ni sawa, bali kuna mengine yake, mengine yake. Hilo ndilo tunalotaka, mengine, naam.

83 "Wakijifunza sikuzote, wasiweze kamwe kuufikia ujuzi wa kweli. Wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, na wasiowapenda walio wema." Mliona jambo hilo? Mwanzoni mwa huo mlango, alisema, "Roho anena waziwazi, ya kwamba katika siku za mwisho," hiyo ndiyo ingekuwa hali. "Katika siku za mwisho, watu wanapaswa kuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kiburi, wenye kujisifu, wenye kukufuru," loo, "wasio safi, wasio na upendo wa asili," si hata upendo wa asili, "wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wasiowapenda walio wema, wenye mfano wa utauwa," sasa, hilo ni Neno la Mungu, Nalo halina budi kutimia, "wenye mfano wa utauwa, bali wakikana nguvu zake."

84 Hivi hamwoni, wameondoka kwenye sauti hiyo inayojulikana, wakachukua sauti isiyojulikana. Wakaingia, wakasema, "Ninii . . . Tulijiunga na kanisa, tukabatizwa, na tukaandika jina letu kwenye kitabu." Sasa, hiyo ni sauti isiyojulikana.

85 Na mmojawapo wa unafiki mkubwa sana ulimwenguni ni kuwa na sauti inayofanana sana na sauti halisi, nayo ina ya kutosha tu juu yake isiwe sauti sahihi. Uongo mkubwa sana uliowahi kusemwa, ni ule ulio na ukweli mwingi sana kwake, halafu moja kwa moja mwishoni, una uongo. Hivyo ndivyo Shetani alivyomwambia Hawa, alidanganywa nao. Huyo mwanamke hakukusudia kudanganyika, bali alidanganywa kwa sababu lilisikika la kweli sana. Mnaona?

86 Basi wanapokwambia, unaweza tu kujiunga na kanisa na uwe sawa, ama kunyunyiziwa, ama kubatizwa kitu fulani, ama kufanya *jambo fulani*, litakuwa sawa, hilo—hilo silo, ndugu, mtu hana budi kuzaliwa mara ya pili kwa maji, na kwa Roho, na kujazwa na Roho Mtakatifu. Mnaona? Ndipo yeye ni kiumbe kipya, ndipo una sauti ya hakika inayosikika sawa.

87 Sasa, sauti inapoingia, hubadilisha hali ya kusikia masikioni mwako. Unaona? Hapo awali, usingeweza kuisikia, sasa unaweza kuisikia. Mtu fulani akihubiri kuhusu uponyaji wa Kiungu, nguvu za Mungu, ungeketi pale tu pasipo kutahiriwa masikio kabisa, usingeweza kusikia chochote, "Mchungaji wangu haamini hilo. Ninaamini huo ni ulokole." Lakini sauti nyingine inapokuja, kama upepo wa nguvu ukienda kasi, na kuyatahiri masikio hayo, basi hiyo ni sauti nzuri, unapoanza kuisikia sauti hiyo ya ninii wenye nguvu unaoenda kasi . . .

88 Loo, muda si muda wajua, inaleta chemchemi za furaha nafsini mwako, nawe unapiga makelele, "Amina. Hiyo ni kweli. Lihubiri, Ndugu. Haleluya! Hilo ni zuri." Mnaona? Inakufanya usogee basi, unaenda mahali fulani.

89 Lakini siku hizi, ni ninii tu, "Jiunge na kanisa." Mnaona, ni sauti isiyojulikana. "Wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa

kuliko kumpenda Mungu," hiyo ni Timotheo wa Pili 3—Timotheo wa Pili 3:7, "wakijifunza sikuzote, wasiweze kabisa kuufikia ujuzi wa kweli." Mnaona? Wakijifunza sikuzote, wakijifunza sikuzote, ndugu, tuna seminari, na shule, na ma-Ph.D., na ma-Dh.D., na ma-D.D.D., na ma-Q.S.T., na kila namna ya kila kitu, "wakijifunza sikuzote, ila wasiweze kabisa kuufikia ujuzi wa kweli." Hiyo ni kweli. Ana digrii ya udaktari, nasi tunamtuma mtoto wetu, na, kwe—kwenye seminari mahali fulani, na kujipatia digrii kubwa ama *kitu kingine* kama hicho, naye anatoka na—na ange—a—a . . . bado kuna kasoro.

90 Huwezi . . . Sasa, kile tunachohitaji siku hizi, na hebu ninyoshe tamshi langu, leo, kuhubiri, mhudumu, mhubiri wa injili, si mtu zaidi sana angeweza kuwa . . . angaliweza kuwa na hii na awe mhubiri, bali tunategemea sha—shahada tuliyo nayo, jinsi tulivyopata Shahada yetu ya Sanaa, na jinsi tulivyochukua Biblia, na kujifunza *hili*.

91 Ibilisi anajua mengi kuhusu Biblia kuliko mtakavyowahi kujua, nitawaambia hilo sasa, yeye anajua yote kuihusu. Hao, baadhi ya wanafunzi bora sana wa Biblia niliopata kukutana nao, walikuwa ni makafiri, wanaisoma tu mchana na usiku, hiyo ni kweli, wapate kubishana nawe kuihusu. Sivyo, Biblia si ya kubishaniwa, Biblia ni ya kuishiwa. Mnaona, kama ukiiweka Mbegu hiyo kwenye udongo usio na rutuba haitaishi, bali ukiiweka katika ardhi yenye rutuba itaishi.

92 Hivi mlisoma, hapa si muda mrefu uliopita, jinsi walivyoenda na kuchukua baadhi ya hiyo ngano kutoka kwenye ghala huko Misri, iliyowekwa mle ndani na Yusufu? Wakachukua mbegu ya alizeti yenye umri wa miaka elfu nne, mbegu ya alizeti yenye umri wa miaka elfu nne, wakaipanda ardhini, ikazaa alizeti. Amina. Ngano ilizaa ngano. Kwa nini? Ilikuwa imerutubishwa, chembechembe hiyo haifi, mnaona, iko mle ndani.

93 Haidhuru wanakuweka wapi, kama umezaliwa mara ya pili, na kujazwa na Roho Mtakatifu, huenda usiwe ninii—hata ninii . . . majivu ya kutosha kushikilia kwenye ukucha wako mdogo wa mkono, bali utafufuka tena katika ule ufufuo, kwa sababu una Uzima, umetiwa nguvu, na, kutoka Juu, na kuna Uzima ndani yako. Kuna sauti iliyotukia, sauti, sauti ya hakika ambapo ulijua kilichotukia, ulikufa na ukazaliwa mara ya pili, ukawa kiumbe kipya.

94 Sauti zisizojulikana, sauti isiyojulikana ya hizo kazi, kutokuwa na uhakika katika mambo ya kitaifa, kutokuwa na hakika katika siasa, kutokuwa na hakika nyumbani, ndipo unaweza kuniambia, "Ndugu Branham, unasema kila kitu kina mashaka. Kwani hakuna chochote cha hakika?" Naam, kuna jambo moja ambalo ni la hakika. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . ? . . . Ni cha kweli Milele. Ni cha hakika Milele.

Loo, kamwe huwezi kuliondokea, ni. . .[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .mlango, Yesu alisema, kifungu cha 35, Yeye alisema, "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe." Basi ni cha hakika Milele.

95 Sasa, mnaona, hatuwezi tena kuweka matumaini katika mambo ya kitaifa, na kazi, ama katika siasa, na katika madhehebu yetu, na kadhalika, lakini kuna jambo moja ambalo ni la hakika, hilo ni Neno la Mungu na ahadi ya Mungu, Mungu anaposema jambo lolote, hilo latosha milele.

96 Hapa wakati fulani uliopita, walijaribu kusema ya kwamba—ya kwamba Mungu alifanya makosa mengi sana. Mnajua, walisema kwamba wakati Daudi alipokipiga kinubi chake, sayansi, walijaribu kabisa kuthibitisha ya kwamba hapakuwapo na kitu kama kinubi katika siku za Daudi, hawakuwa na vinubi, lakini, hatimaye, wakachimbua ushahidi fulani kwamba vinubi vilikuwapo.

97 Kasema wakati Ibrahimu alipowachukua ngamia wake na kushuka kwenda Gerari, walisema ya kwamba hapakuwapo na ngamia kule chini, lakini hapa, hivi majuzi tu, walichimbua mifupa fulani wakaona kulikuwa na ngamia kule chini. Mnaona?

98 Kwa hiyo, walisema ya kwamba Biblia si ya kweli, walikuwa waende wakachimbue chini waone kile, kile wanachoita bustani ya Edeni, kuthibitisha ilikuwa tu ni mwanzo wa ustaarabu, mahali fulani, nao walipochimba chini, wakijaribu kukanusha Biblia, walichimbua ninii. . .juu ya mwamba, ambapo ilikuwa imeandikwa, ambapo Isaya alimponya Hezekia majipu. Kuthibitisha tu ya kwamba. . .

99 Nao walisema ya kwamba kuta za Yeriko hazikuanguka chini, hakukuwako na kitu kama hicho, wakachimba kila mahali pale, wala hapakuwapo na kitu kama kuta. Kisha daktari fulani akashuka akaenda kule na kuchimba chini, chini, chini, ndipo akagundua, hizo hapo, futi ishirini ama thelathini chini ya mahali wa—walipokuwa wakichimba, na hizo hapo, zimelundikana, jinsi hasa Biblia ilivyosema. Kwa hiyo Mungu alikuwa sahihi hata hivyo. Hmm!

100 Walisema huko nyuma, babu wa babu wa babu yako, iwapo alikuwa mkosoaji, alisema, "Hakuwezi kuwa na gari linaloenda bila kufungiwa farasi." Lakini tunalo hata hivyo. Hiyo ni kweli. Na mambo haya yote ambayo Mungu alinena habari zake, hayo ni ukweli wa Milele.

101 Hapa wakati fulani uliopita, ilihojiwa kuhusu Sulemani katika Biblia, aliposema, "Aonavyo mtu moyoni mwake, ndivyo alivyo." Vema basi, huyo mwanasayansi akasema, "Angalia hapa, hakuna akili katika moyo wa mwanadamu, Sulemani alimaanisha kichwa chake." Huh! Kama angalimaanisha *kichwa*, angalisema, *kichwa*, hivyo ndivyo ilivyo. Ni—ninaamini Biblia kuwa jinsi hasa ilivyoandikwa. Ninii tu, ninaamini Hilo

ni Neno la Mungu, ninii tu, ninaamini ni Mungu. Mungu si bora kuliko Neno Lake, wewe si bora kuliko neno lako. Neno lako mwenyewe ndilo litakalosimama pale kukuhukumu kwenye Siku hiyo.

102 Sasa, huko Chicago yapata miaka minne iliyopita, msichana mdogo wa Ndugu Mattsson-Boze, Joyce, ataolewa mwezi ujao, msichana mdogo wa kupendeza, daima ananiambia jambo fulani, na kucheka, kila mara huwa tu na utani mdogo wa kuniambia, akisema juu ya jambo fulani ambalo—ambalo ni ki—kichekesho kidogo kinachombidi kutoa kuhusu jambo fulani, ndipo ananiambia, akasema, "Je, ulisikia kilichokuwa gazetini leo?"

Nami nikasema—nikasema, "Sasa, ngoja kidogo, Joyce, sasa uta—utaniambia nini sasa? Nini . . . ?"

103 Kasema, "La, huu sio, Ndugu Branham," kasema, "nitakuletea, nikuonyeshe." Kasema, "Nilikusikia ukisema juu ya mtu kuwazia moyoni mwake." Nililisoma katika Biblia. Akasema, "Sasa, leo wamegundua, na kuthibitisha, hakiko ndani ya, hakiko katika moyo mwingine wowote, bali moyo wa mwanadamu, hakiko katika moyo wa mnyama, lakini kuna chumba kidogo moyoni ambacho sayansi inasema ni mahali ambapo nafsi hukaa." Kwa hiyo basi Mungu alikuwa sahihi aliposema, "Kama vile mtu aonavyo moyoni mwake." Mnaona, kuna chumba cha kiakili moyoni.

104 Sasa, unaposema, "Vema sasa, mimi—mimi—mimi . . . " Je, uliwahi . . . ? Ninyi nyote mmekuwa na jambo hili: nyakati ambazo mngewazia, "Vema, si—sijui kama lingeweza kutukia ama la." Na kwa ghafla *kitu fulani* kinakwambia tu, "Itatukia," haidhuru mtu mwingine yeyote anasema nini, unajua litatukia. Sote tumekuwa na matukio hayo. Hapo ndipo moyo wako unapowazia, hapo ni moyo wako ukikwambia.

105 Sasa, akili hutoa hoja, bali moyo hautoi hoja, unaamini tu. Laiti ningaliweza kulielekeza hilo nyumbani kwa mmoja wa wasikilizaji wangu, ningekuwa na ibada halisi ya uponyaji, kama ningeweza kuwafanya wasikilizaji wangu waone hilo, kwamba si kile kichwa chako kinachowazia hata kidogo. Hapo ndipo ibilisi anapokaa, bali yeye hulihoji, "Mi—mimi ni mgonjwa, siwezi kupona. Ni—nina *hili*," ama, "Siwezi kuokoka, ni—ni—nimefanya mengi kupita kiasi." Mnaona, hiyo ni *hoja*, bali inatupasa kutupilia mbali hoja. Hiyo ni kweli. Tukitupa chini hoja zetu, tunaamini kwa moyo wetu.

106 Katika bustani ya Edeni, mwanadamu aligawanyika katika sehemu mbili, ibilisi akachukua kichwa chake, na Mungu akauchukua moyo wake. Ibilisi humfanya aangalie mambo, na kusema, "Vema, kamwe haliwezi kutukia, ninaweza kulihoji." Naye Mungu akauchukua moyo wake akae moyoni mwake kumfanya aamini mambo ambayo kichwa chake hata hakijui

chochote kuyahusu. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo ni katika moyo wako unawazia. *Hapa* chini, hapo ndipo Sauti halisi ya hakika inapotoka, ni kutoka moyoni, hapo ndipo Mungu huzungumza, na *hapa* ndipo ibilisi anapozungumzia. Kwa hiyo hebu na tutupe chini yale ibilisi aliyosema, na tuchukue Sauti ya hakika, na Sauti hiyo ya hakika ni Mungu akinena moyoni mwetu, hiyo ni kweli, ahadi za Mungu.

107 Hebu tuhojiane tu kwa dakika tatu ama nne zijazo, tuone baadhi ya waliozichukua ahadi Zake, na kama zilikuwa za kweli ama si za kweli. Hawakuzihoji. Mungu anakufanya uwazie mambo, na kufanya mambo yasiyo na maana kwa kichwa cha mwanadamu. Mlijua hilo?

108 Huyu hapa mvulana mdogo ameketi hapa kwenye kiti, kiti cha magurudumu, labda, huenda ikawa mama na baba yake walimleta, naye . . . labda madaktari walimfanyia kila kitu wawezacho kumfanyia. Mnaona? Akasema, "Yote yamekwisha." Vema sasa, kama utasikiliza yale anayokwambia, basi yote yamekwisha, lakini kama kuna kitu kinachoanza kutenda kazi *hapa* chini, ndugu, hiyo—hiyo ni tofauti basi, hiyo ni sauti nyingine.

109 Sasa, sauti *hii* inasema, "Imekwisha." Lakini sauti *hii* ni sauti ya hakika, itaikana *hii*. Sasa, inategemea . . . Na *hii* itajaribu kuikana *ile*, vinginevyo. Lakini inategemea ni ipi unayosikiliza.

Kama vile yule Mhindi alivyokuwa wakati huo, aliyeokoka. Kasema, "Unaendeleaje, Chifu?"

110 Kasema, "Vema, tangu nilipookoka, kuna mbwa wawili ndani yangu, na," kasema, "mmoja ni mweupe na mmoja ni mweusi, na yule mweupe anataka nitende mema, na mweusi anataka nifanye mabaya." Kasema, "Wanapigana wakati wote."

Akasema, "Vema, u—unaendeleaje? Ni yupi anayeshinda, Chifu?"

111 Anasema, "Inategemea ni yupi Chifu anamlisha zaidi." Vema, ndivyo hivyo. Kama utasikiliza hoja, sikuzote utamfanya *huyu* jamaa kushindwa, lakini kama utasikiliza ile Sauti ya hakika, Neno la Mungu, akifanya kazi moyoni mwako, utamshinda *huyu*. Unamlisha yupi?

112 Usisikilize sauti isiyojulikana, kwa sababu tuna ushahidi mkamilifu kote katika kila wakati kwamba Mungu hufanya miujiza, hufanya mambo ambayo sayansi haijui kitu kuyahusu. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo usiyazingatie yale jamaa *huyu* asemayo, wakati jamaa *huyu* anapoanza kuzungumza, acha jamaa *huyu* aondoke njiani. Sawa.

113 Sasa, tunachukua kwa mfano, watu wawili au watatu tu katika Biblia waliosikiliza, na kamwe hawakuzungumza hoja zao, walizungumza na ninii yao, sauti *hii* ya hakika.

114 Mungu alikutana na Nuhu, Naye akasema, "Nuhu, itanyesha, nami ni—ninataka ujenge safina sasa, kwa ajili ya ukombozi wa nyumba yako." Sasa, hivi mlijua kamwe haikuwa imenyesha hata tone moja duniani mpaka wakati huo? Kamwe haikuwa imenyesha. Sasa, ungeweza kuwazia, wakati sayansi . . .? Mnasema, "Hakukuwako na . . . " Loo naam, kulikuwako, pia, walitoka kwenye ukoo wa Kaini, naam, bwana, wanasayansi mashuhuri, mbali zaidi na yale tuliyo nayo siku hizi, sayansi kuu zaidi.

115 Walijenga Sfiniksi na piramidi katika siku hizo, hatuwezi kufanya hivyo siku hizi. Walikuwa na nyenzo zilizokuwako, nao walikuwa na nguvu zilizozidi chochote tulicho nacho, isipokuwa iwe ni za atomiki, walikuwa wakiitumia. Nao walifanya vitu ambavyo hatujui chochote kuvihusu. Wangeweza kufanya mumiani katika siku hizo, tusingeweza kuufanya hata tufanyeje, hakuna kitu kama cha kutengeneza mumiani siku hizi, lakini waliutengeneza. Mnaona? Wangeweza kuifanya maiti isioze kwa njia fulani na kuifanya ionekane ya kawaida kabisa mpaka wa leo, maelfu ya miaka baadaye, hatuna hiyo. Walikuwa na rangi ambayo ingedumu, na vitu vingi tu pale ambavyo hatuna, sayansi yao ilikuwa imeendelea kuliko yetu.

116 Sasa, huenda sayansi ilisema, "Sasa, ninataka kukuuliza jambo fulani. Hayo maji yanatoka wapi kamwe? Ninaweza kuona kote kote hata kwenye nyota, ninaweza kuona kote hata mwezini, ninaweza kuona kote hata kwenye jua, tuna vyombo hapa vinavyoweza kurusha ujumbe mwezini, tunaweza kwenda kwenye nyota twende kwenye Mirihi, vitu kama hivyo, niambie mahali maji yalipo, tafadhali, Bw. Nuhu."

117 "Vema, nitakwambia, nilisikia Sauti siku moja, Nayo ilikuwa ni Sauti ya Mungu iliyoniambia nijenge safina. Nami . . . Kwa hakika tu kama vile kulivyo na ulimwengu tunaoishi, Mungu atauangamiza kwa maji. Nayo itanyesha moja kwa moja kutoka kwenye mbingu ile, Mungu anaweza kuyaweka huko juu. Kama alisema itakuja, atafanya njia ya jambo hilo." Hiyo ni kweli.

118 Sasa, kama isingalikuwa na hakika, na kujua ya kwamba sauti hiyo ilikuwa ya hakika, mkosoaji wa kwanza, angesema, "Vema, labda mimi—labda nilielewa vibaya." Hivyo ndivyo watu wanavyofanya siku hizi.

Daktari anasema, "Huna nafuu hata kidogo."

"Vema, labda nilielewa vibaya. Labda, mi—mimi . . . " Loo, jamani! Unaona? Lakini kama una hakika na sauti hiyo ya hakika!

119 "Kama baragumu ikitoa sauti isiyojulikana ni nani anayeweza kujiandaa kwa vita?" Kama haijulikani, askari angefanya nini, ka—kama ilikuwa, walikuwa wakijiandaa kwa vita, na—nao walitoa sauti, wala haikusikika kama tu sa—sauti

ya kawaida ya kwenda vitani? Asingejua kama arudi nyuma, kama aende vitani, ama aketi chini, ama—ama ale chakula chake cha jioni, au la kufanya, ama kwenda kitandani, kama haikutoa tofauti halisi katika hiyo sauti.

120 Kwa hiyo, Neno la Mungu halileti mashaka yoyote, linatoa sauti ya hakika, sauti ya hakika. Mungu anapozungumza na mtu binafsi, ni hakika, sijali yale mtu mwingine yeyote asemayo, yale sayansi isemayo, yale taifa lisemayo, yale ulimwengu usemayo, yale kanisa lisemayo, yale mtu mwingine yeyote asemayo, ni ya hakika. Neno la Mungu ni Sauti ya hakika; kila mtu aliyepata kuisikia na kuitii alifanya jambo fulani, pia.

121 Sasa, Nuhu, akiisha kuonywa na Mungu, alienda, na kutengeneza safina kwa ajili ya ukombozi wa nyumba yake. Hiyo ilikuwa ni sauti ya hakika, Mungu alisema itanyesha, na ikanyesha, ndipo wale waliopata njia ya kuepukia, wakaichukua; wale ambao hawakuipata, wakaangamia.

122 Mungu yeye yule aliyesema, "Itanyesha," alisema, "Moto utashuka kutoka Mbinguni na kuuangamiza ulimwengu. Na kuna njia iliyoandaliwa kwa ajili yenu, wale watakaoichukua wataepuka, wale wasioichukua wataangamia." Mwenye dhambi ataangamia pamoja na ulimwengu wenye dhambi, bali waliokombolewa watakombolewa na Roho Mtakatifu.

123 Nuhu alisimama moja kwa moja mlangoni mwa safina, na kuleta hukumu juu ya nchi, akawahukumu hao watu, kwa sababu hawakuamini huo Ujumbe, yale Mungu aliyokuwa anaenda kufanya. Naye akaleta ghadhabu ya Mungu juu ya nchi kwa kusimama mlangoni pa safina yake na kuhubiri kuhesabiwa haki. Akasimama mlangoni na kulitangaza Neno la Mungu, kwa sababu lilidhihirishwa kwake kama Sauti ya hakika, ya kwamba Mungu alikuwa anaenda kufanya jambo fulani.

124 Usiku wa leo, kama ndugu yenu, ninasimama mlangoni mwa Safina hii, Kristo Yesu, na kuwatangazia ya kwamba Yeye ni Mwokozi, Mponyaji, Mfalme ajaye. Na kutokana na jumbe hizi za wahudumu mlangoni, ataleta ghadhabu ya Mungu katika hukumu juu ya mataifa, juu ya ulimwengu. Ni Sauti ya hakika, tunaijua Hiyo, ni Neno la Mungu. Na wote wasiomtafuta Kristo kwa ajili ya wokovu wataangamia, wale watendao dhambi wataangamia pamoja na dhambi; wao ni wa ulimwengu, wataangamia pamoja na ulimwengu.

125 Nuhu alielea juu yake katika safina yake, kwa sababu alisimama kwenye mlango wa maandalizi ya pekee Mungu aliyokuwa nayo ya kuepukia. Nami ninasema leo, ya kwamba kanisa lako halitakuokoa, kanuni yako ya imani haitakuokoa, itahitaji Mungu kukuokoa, Roho Mtakatifu, nawe umebatizwa na Roho Mtakatifu katika Safina ya Kristo Yesu, "Kwa kuwa kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja," Kitu cha pekee kitakachokuokoa. Lisikieni! Usichukue sauti

isiyojulikana: "Mimi ni Mmethodisti," "Mimi ni Mbaptisti," na, "Mimi ni Mpentekoste," "Nimefanya *hivi*, nimefanya *hivi*, mimi . . ." Usichukue hiyo, hiyo ni sauti isiyojulikana; lakini Mungu anapoingia, hiyo ni sauti inayojulikana, mnajua habari zake, sote mradi tu unaishi katika dunia hii, bado utaijua, ni jambo linalokupata.

126 Ilikuwa ni sauti ya hakika, ilimfanya Nuhu kutenda kiwazimu kabla haijadhihirishwa, kabla haijatimia, vivyo hivyo na Kanisa siku hizi, linalomkubali Kristo, na limezaliwa na Roho Mtakatifu, watu wanafikiri watu hao wana kichaa, baadhi yao wanasema, "Ndugu Branham, wewe ungali ni Mbaptisti?"

Nikasema, "La, mimi ni Mpentekoste."

"Ati *nini*?"

Nikasema, "Mpentekoste."

"Unamaanisha nini?"

Nikasema, "Ni—nimezaliwa kwa Roho wa Mungu, na kumpokea Roho Mtakatifu." Nikasema, "Mimi ni Mpentekoste."

Kisha kasema, "Ai, uliingia wazimu."

127 Nikasema, "La, nilisikia tu sauti ya hakika, nayo, hapa ndipo ilipotoka, ililia moja kwa moja kutoka kwenye kurasa za Biblia hii, dhahiri tu kama kengele. Nilipoipokea, ninajua kilichotukia, nilikuwako, najua ilitukia." Hakika, ilinibadilisha kutoka mautini kuingia Uzimani, ilinifanyia jambo fulani, ni sauti ya hakika. Hiyo . . .

128 Najua mimi ninatenda kiwazimu kwa watu, nawe ungetenda kiwazimu kwa watu, pia, ninyi ambao mmempokea, bali tunajua mahali tunaposimama, tunajua kile tunachozungumzia, ni sauti halisi. Ni sauti ile ile tu iliyokuja katika Biblia, inatufanya tutende vivyo hivyo, itamfanya mtu mweusi, mtu wa manjano, mtu wa hudhurungi, wote watende vivyo hivyo, kwa sababu ni sauti ile ile. Amina. Sauti ya hakika.

129 Baragumu inatoa sauti isiyojulikana, vema, ningekuwa Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresbiteri, Mpentekoste kwa jina, ama chochote kile, mnaona, hakuna uhakika wa jambo hilo, lakini wakati sauti hiyo ya hakika inapokuja, basi unaijua, ni sauti ya hakika.

130 Sasa, vipi kuhusu Nuhu akisimama pale, akihubiri sana ya kwamba itanyesha? Mbona, watu walimcheka, lakini siku moja ilidhihirika. Hiyo ni kweli. Nuhu aliendelea kupigilia moja kwa moja, akasimama moja kwa moja, kisha akaendelea tu kuweka mbao, akipigilia, ndipo akatoka huko nje na akaipaka lami safina, akaitia lami.

131 Sasa, ilitengenezwa kwa mshita, na ukiangalia huo ndio mti mwepesi kuliko yote iliyopo, ni mwepesi kuliko balsamu. Na huo ndio umeijenga safina, huo ndio—huo ndio uliojengewa, mbao

za safina hii. Imetengenezwa kwa mbao nyembamba, mbao nyepesi. Wangefanya nini nazo? Hawana budi kutoa utomvu wote kutoka kwake, na kuufanya mwepesi, waukaushe, mpaka utakapokauka kabisa, na ndipo unanyumbulika, unaweza kuutumia.

132 Sana sana ndani yetu, kila tunapoanza kuinama, tunavunjika. Lakini inakubidi kuondoa u—utomvu wote wa kilimwengu kutoka kwako, ulimwengu wote utolewe ndani yako, kisha uushikilie juu ya moto, moto utavuta na kutoa huo utomvu. Nami nawaambia, hilo ndilo linalohitajika kutoa utomvu kutoka kwetu sasa, utomvu wa kilimwengu.

133 Basi walifanya nini nayo? Walichukua mti na kukata msandarasi, na badala ya—ya kuuangusha chini tu, waliuchukua na kuupiga, nao wakaupiga huo mti mpaka ulimbo ukatoka ndani yake. Ndipo wakatoa ulimbo kutoka kwenye huo, wakaumwaga kwenye mbao hizi za mshita, basi walipofanya hivyo, ulijaza nyufa hizi zote na ni mgumu kuliko feleji, hiyo ni kweli, ndipo zikawa katika safina. Naye Mungu akaipaka rangi kwa nje, ama—ama, Nuhu akaipaka, ndani na nje, akaipaka. Vema, hivyo ndivyo hasa Mungu alivyomwambia aijenge.

134 Na hivyo ndivyo tunavyoijenga siku hizi. Hatuwezi kumwaga maji haya na kadhalika Kanisani na kulifanya chochote. Unaweza kubatizwa kifudifudi, kinyumenyume, vyovyote utakavyo, haitafaa kitu, hata kidogo. Tunabishana kuhusu kanuni za imani, kuhusu kunyunyizia, kuhusu kumwagilia, kuhusu *hili*, *lile*, na *linginelo*. Vema, yafaa nini kama hayo tu ndiyo mliyo nayo? Hiyo ni kweli.

135 Nami nilisema ya kwamba sijui kama waliwahi. . . Ilikuwa wakati mmoja nilipokuwa mvulana mdogo, kulikuwa na. . . Mimi na ndugu yangu tulikuwa huko nyuma ya shamba, na kulikuwa na. . . tukamwona maskini kasa, naye alikuwa. . . mnajua jinsi wanavyotembea na miguu yao namna *hiyo*, vitu vinavyoonekana vya kuchekesha. Nami na Ndugu tukawazia huyo alikuwa ndiye kiumbe cha kuchekesha kuliko vyote tulichopata kuona. Kwa hiyo, nilipomkaribia kabisa, akafanya *chweee!* Akarudi ndani yake namna *hiyo*.

136 Kama tu, unajua, ukianza kuhubiri Injili, ukiishindilia kwelikweli, utawaona maskini hao kasa wakininii tu, mwajua, wakijirudisha kwenye ganda, "*Baa!* Nitashuka tu kwenye *Ninii*." Um-hum. Naam.

137 Ndipo nikamwendea, nikasema, "Sijui kama tungeweza kumfanya atembee." Vema, tu—tukambana, nasi tulifanya yote tuliyoweza, a—asingetembea. Tulimsukuma, tukampiga mateke pande zote, halikumfanya atembee. Vema, nikaenda nikajichukulia mjeledi, nami nikamcharaza kwelikweli, wala ha—hakutembea. Basi nikasema, "Vema. . . " Nami. . . Jambo ndilo hilo, hu—huwezi—huwezi kumcharaza atembee.

138 Kwa hiyo, basi nikasema, “Ni—ni—nitamkomesha, Ndugu.” Tukaenda kwenye chemchemi kule chini, na, kwenye shimo la maji, nikamtumbukiza tu mle ndani, nikasema, “Nitamzamisha, la sivyo atatembea.” Nami nikamshikilia kule chini, ndipo mapovu machache tu yakatokea na ni hayo tu, alikuwa tu sawa. Ndugu, wewe. . . maji hayafai kitu.

139 Lakini mnajua jinsi nilivyomfanya atembee? Niliokota kipande cha karatasi, nikawasha moto mdogo nikamlaza juu yake, ndugu, alitembea wakati huo. Naam.

140 Kama kuna jambo lolote litakalolifanya Kanisa litembee sawa, litende haki, lijionyeshe, ni ubatizo wa Roho Mtakatifu na Moto ukishuka kutoka kwa Mungu Mbinguni utalinyosha Kanisa, sio kuzozania *hili*, wala kuzozania *lile*, bali ni kushuka kwa ubatizo wa upendo wa moto wa Mungu, na kufagilia mbali hivyo vitu kutoka moyoni mwako, kukufanya kiumbe kipya katika Kristo Yesu. Wanawake wataacha nywele zao zikue, nao wanaume wataacha kuvuta sigara, nami nawaambia, na, mambo haya yote yatanyooka, kama tu mkishusha Moto juu yao. Kweli.

141 Sasa, lilionekana la kigeni sana kwa Nuhu wakati alipokuwa akifanya jambo hili, bali alikuwa. . . alisikia sauti hiyo ya hakika, hiyo ndiyo aliyotaka.

142 Sasa, hebu na tuchukue jamaa mwingine, kulikuwa na mtu ji—jina lake Musa, alikuwa upande wa nyuma wa jangwa, amejaa mafundisho kadiri alivyoweza kuwa. Yeye alijua mambo yote ya—ya ndani na nje, hata angeweza kuwafundisha Wamisri, watu werevu sana ulimwenguni, angeweza kuwafundisha theolojia. Lakini siku moja huko nje, a—aliona kitu fulani kikiwaka Moto, na kidogo kikamvutia.

143 Hilo ndilo linalohitajika siku hizi, ni Kanisa linalowaka Moto kuwavutia baadhi ya hawa akina Musa hapa mahali fulani, kuwavutia baadhi ya hawa wenye dhambi, inahitaji Moto kutoa mvuto. Hebu ma—ma—mayowe yatokee mtaani ya “Moto!” ninii halisi. . . kila mtu aruke aingie kwenye gari lao, na kujaribu kuyafuatilia. Kuna kitu kinachovutia kuhusu moto. Tunachohitaji usiku wa leo ni Roho Mtakatifu na Moto, ambao utamvutia mwaminio anayeona kitu fulani.

144 Ninamkumbuka rafiki yangu wa kale jina lake Ben Pemberton. Loo, yeye ni jamaa kwelikweli! Huko St. Louis, alikuwa na mkutano wa hema ukiendelea huko chini, wala hakuna mtu angeuhudhuria, kwa hiyo akakimbia mbio kidogo mtaani, papo hapo katikati ya mji, naye akasema kwa sauti kuu, “Moto! Moto! Moto! Moto!” Naye huyo akapanda barabarani akiitikisa kofia yake kwa nguvu alivyoweza. Alikuwa na hema huko juu, ndipo kila mtu akaanza kukimbia aone huyu jamaa mwenye kicha alikuwa na shida gani. Akakimbia kule juu, na kuruka juu ya mi-. . . kisha akushuka moja kwa moja, alikuwa ni mcheshi tu, kitu kama hicho, akashuka moja kwa moja, na

kuruka mimbarani, akasema kwa sauti kuu, "Roho Mtakatifu na Moto!" Ndipo akaanza kuhubiri kwa nguvu tu alivyoweza. Hiyo ni . . . Mnaona, kitu fulani, kuvutia usikivu. Na kitu bora sana cha kumvutia mtu mkaidi ni Roho Mtakatifu na Moto. Hivyo ndivyo Mungu alivyofanya.

145 Sasa, Musa hakufikiri angeweza kufanya hivyo. Alijaribu jambo hilo kwa msimamo wake wa kimafundisho, wala halikufaa kitu. Lakini Mungu, siku moja, alinena naye, na kusema, "Vua viatu vyako, Musa, ninajua wewe ni mwana mfalme huko Misri, lakini wewe si kitu machoni pangu. Vua viatu vyako, uko kwenye mahali patakatifu. Ondoa yote, ondoa upuuzi huo wote ulio nao ndani yako." Naye akasikia sauti. Akasema, "Nitakutuma huko chini ukawakomboe watu Wangu." Sasa, haikuwa isiyojulikana.

146 Sasa, Musa alijuaje hiyo haikuwa isiyojulikana? Vipi kama angalisema, "Ni nani huyu anayezungumza nami? Ni kitu gani?" Kwa sababu ile Sauti iliyonena naye iliambatana kabisa na Maandiko. Hivyo ndivyo unavyojua kama ni sauti inayojulikana au la, ama sauti isiyojulikana. Kama Maandiko . . . Kama sauti inayokuzungumzia si ya Kimaandiko, basi usiisikilize. Unaona? Lakini iwapo ni ya Kimaandiko, isikie, maana ni Sauti ya Mungu. Unaona? Akasema, "Nimesikia kilio cha watu Wangu, na nimeona ninii yao . . . mateso yao, na wanyapara wao, yale waliyofanya, nami nimeikumbuka ahadi Yangu na agano Langu." Mnaona?

147 Musa akasema, "Hayo ni Maandiko hasa." Sasa, hivyo ndivyo unavyotaka kufanya, kusikia ina sauti ya namna gani, uone kama ni sauti ya Kimaandiko. Kama ni sauti ya Kimaandiko, basi ni sauti ya hakika, kwa sababu ahadi za Mungu ni kweli. Kama Biblia . . .

148 Kama ukimsikia maskini msomi fulani aliyetoka kwenye seminari, na kusema, "Aa, hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu, huo wote ni msisimko." Sikiliza, ndugu, hiyo ni shaba iliayo na upatu uvumao, usisikilize hayo. Naam, bwana.

149 Lakini unapomsikia akisema, "Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele," hiyo ni—hiyo ni sauti ya hakika, hiyo—hiyo ni kweli kabisa, "Mimi ni Bwana, niponyaye magonjwa yako yote," hiyo ni sauti ya hakika. Unaona? Sasa, sikilizeni sauti ya hakika, si isiyojulikana.

150 Sasa, ndipo Musa akashuka na kuwakomboa hao watoto, kwa sababu alikuwa na sauti inayojulikana. Watoto wa Kiebrania walisikia sauti inayojulikana, hapana shaka, usiku huo katika mkutano wa maombi, "Mungu wetu anaweza kutukomboa, hata hivyo, hatutachukua kitu kingine chochote ila Neno Lake. Tunasimama waaminifu Kwake kabisa, haidhuru ni kitu gani kinachotukia, tunaenda . . . " Ilikuwa

ni sauti inayojulikana. Hiyo ni kweli. Wanajua walichokuwa wakizungumzia.

151 Ibrahimu, mkulima, mwenye umri wa miaka sabini na mitano, labda alikuwa kafiri, alishuka kutoka kwenye mnara wa Babeli ambako walikuwa na huo ushirikina wote kule juu, na kadhalika, lakini siku moja alipokuwa akifanya kazi shambani, alisikia sauti, nayo ilikuwa ni sauti inayojulikana. Miaka ishirini na mitano baadaye, pasipo na ushahidi kwamba sauti hiyo ingeweza kudhihirishwa, aliiamini mara mbili tu ya alivyoiamini hapo mwanzo. Haya basi.

152 Mungu akasema, "Ibrahimu, utakuwa na—utapata . . . mkeo atapata mtoto. Na—naye ana umri wa miaka sitini na mitano sasa, nawe una sabini na mitano, bali Mimi ni Bwana, ni—nitamchukua mtoto huyo mchanga, na kwa njia hiyo nikufanye baba wa mataifa ya ulimwengu. Nitakufanya tu baba wa mataifa mengi sasa." Ndipo baada ya kitambo kidogo Yeye alikutana naye, na kubadilisha jina lake, na kumwita kutoka kwa *Ibrahimu*, uh, *Abramu*, akawa *Ibrahimu*, akampa sehemu ya Jina Lake, *Elohimu*, na kwa hiyo, maana Yeye alikuwa ni Baba, akamfanya baba wa mataifa.

153 Sasa, Ibrahimu aliendelea tu kuamini ahadi hiyo, mwezi wa kwanza, mwezi wa pili, mwaka wa kwanza, mwaka wa tatu, mwaka wa tano, mwaka wa ishirini na tano, angali aliiamini. Nayo Biblia ilisema ya kwamba hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini, bali alikuwa na nguvu, akimtukuza Mungu. Mnaona? Alisikia sauti ya hakika. Haidhuru inachukua muda gani, hilo halina uhusiano wowote nalo, ni sauti iliyo sahihi, haidhuru ni nini. *Whiu!* Loo, kama mngeweza tu kupata hilo, enyi Kanisa, yote yangekwisha, ninawaambia. Mambo yangekuwa tofauti kama tungeweza tu kupata *hilo*, mnaona, sauti hiyo ya hakika, kwamba ni Mungu. Tunajuaje? Alisema hivyo.

"Unajuaje, Ibrahimu, utampata mtoto huyu kwa Sara?"

"Mungu alisema hivyo."

"Vema, angalia hapa, yeye ana umri wa miaka sitini na mitano."

"Sijali kama alikuwa na umri wa miaka mia sitini. Haidhuru ni nini, Mungu alisema hivyo, hilo latosha."

154 "Nadhani wewe, kama ni . . . Loo, nitaninii, vema, nitakuja huku mwaka ujao nione jinsi—jinsi mtoto huyo anavyoendelea. Baada ya miezi tisa ni—nitarudi kumwona mtoto wako."

"Huenda asiwepo katika miezi tisa, naamini atakuwapo, ila kama hatakuwa hapa katika miezi tisa, huenda ikawa ni tisa inayofuata." Mnaona? "Atakuja."

155 Miaka ikapita, miaka ikapita. Vipi kuhusu hilo? Akapata nguvu zaidi na zaidi, akisema, "Utukufu kwa Mungu! Mungu

alisema hivyo, loo, nisingeweza kutokuliamini hata nifanyeje." Loo!

156 Ilitokea niliangalia papa *hapa* na kumwona Ndugu na Dada Kidd wameketi hapa. Mbona, alisema, si muda mrefu uliopita, mimi . . . daktari mmoja alitoa sauti, mzee huyo alikuwa anakufa, mnaona, nami nusura niichome tairi ya gari langu nipate kufika hapa juu kumwaga kwaheri. Nilipofika mle chumbani asubuhi moja, Roho Mtakatifu akasema, "La, hatakufa." Huyu hapa. Nilisikia ameongezeka ratili ishirini na tano. Jamani, jamani, jamani! Kwa hiyo mnaona hilo? Ni sauti ya hakika, mnaona. Ni uhakika, kama Mungu alisema hivyo, ndivyo *ilivyo*.

157 Nilipokuwa tu nikija kutoka California hivi majuzi, sikuwa nimeingiza sanduku langu, sikuwa nyumbani kwa miezi miwili, kwenye miezi miwili hasa, nikaingiza angalau sanduku la pili, simu ikalia, ilikuwa ni mama fulani. Vema, alikuwa kwa namna fulani rafiki yangu wa kike, miaka kadhaa iliyopita nilipokuwa mchungaji wa Kanisa la Kibaptisti la Milltown.

158 Alikuwa na binti wawili wa kupendeza, naye akaolewa na mtu mzuri, Ndugu Huff, naye alikuwa fundi wa vinu, alivijutia, kimoja cha vidole vyake pamoja na vidole gumba vilikatwa, ndugu mzuri sana. Walikuwa—walikuwa na mapacha—mapacha wawili, na msichana mwingine, wakawa watoto watatu. Nao hao mapacha walikuwa ni Wakristo waaminifu, wa—wao walikuwa ni watu wa UBC, lakini wao—wao kweli wanamwamini Mungu. Na kwa hiyo wao, msichana mmoja mdogo, akienda shuleni, alipata kinyongo, hao wasichana walimwambia, "Vema, kwa nini usivute sigara kama sisi? Kwani unafikiri wewe ni bora kuliko sisi? Kwa nini usiende kwenye madansi?"

159 Sasa, wao hawakwenda kwenye madansi, wala hawakuvuta sigara wala kunywa pombe, nao walimdhihaki. Yule msichana mwenye afya zaidi, alisema, "*Hmm*! Hebu watumbukie mtoni. *Mimi* ndimi ninayemtumikia Kristo, wasipotaka, acha waendelee."

160 Lakini huyo mwingine, akaanza kuwazia, "Loo, labda ningeweza kufanya jambo fulani." Naye akapata kinyongo, akashikwa na wasiwasi, akawa mwendawazimu, wakamlaza hospitalini miaka miwili. Na kwa hiyo, walikuwa wakijaribu kumtibu, kwa kumpa vitu vya kila namna, na matibabu, na—na kila kitu. Wao . . . Haikufanya kazi vizuri.

161 Kwa hiyo basi, nilipofika nyumbani, walisema, "Ndugu Branham, walimpeleka kwenye taasisi ile ya Katoliki kule, halafu Jumatatu watampeleka Madison." Hiyo ni seli iliyofungwa, hiyo inafaa.

162 Ana umri wa miaka kumi na minane, na ni mtu mwenye kipaji, yeye ni mmoja wa watu wa ukamilifu. Hata hufundisha opera, na hucheza yaleli, na hufundisha muziki akiwa na umri wa miaka kumi na minane. Mnaona? Msichana mwerevu tu

kwelikweli. Na kwa hiyo yeye…Mkristo mzuri sana, wala wasingeweza kulielewa.

163 Na kwa hiyo waliposema walikuwa wanaenda kumweka mle kwenye seli iliyofungwa, hilo lilitosha. Wakampa, ninasahau ni matibabu mangapi ya kushtuliwa, na hayo ni matibabu ya kubahatisha, mwajua, na kwa hiyo yakamwathiri zaidi, kwa hiyo daktari akasema, "Hakuna matumaini kwake kwa hiyo tutampeleka Madison, Jumatatu."

164 Na kwa hiyo, maskini mama huyo akasema, "Ninakumbuka jinsi Ndugu Branham, alipokuwa hapa chini kwenye…na alikuwa akitwambia kuhusu Kristo kuwa Mponyaji." Kasema, "Mimi, na nimesikia taarifa za kila namna za magazeti, na kadhalika, kuhusu mahali amekuwa." Walikuwa ni watu wa mashambani, huko nyuma kabisa mashambani, na kwa hiyo, na kusema, "Laiti ningaliweza tu kushika!" Kwa hiyo wakapiga simu Jeffersonville, ofisini, nao wakasema nilikuwa California, nitakuwa nyumbani siku fulani. Kasema, "Vema, hilo litatupa tu… " Nafikiri hiyo ilikuwa ni Ijumaa nilipoingia, hiyo ingekuwa Jumatatu wangemwondoa.

165 Kwa hiyo akaenda na kumwomba daktari kama ningeweza kuja huko, naye daktari akasema, "La. Hasha. Usimchochee." Kasema, "Hakuna kitu anachoweza kufanyiwa," daktari wa akili, na hao wengine kule.

166 Kwa hiyo wakaendelea, naye Ndugu Huff akasema, "Angalia," ilikuwa ni hospitali ya Kikatoliki, kasema, "ndugu yetu ni kama tu kwamba ungempa ibada ya mwisho ama chochote kile, kasisi."

Akasema, "Vema, yeye ni…Hakuna kinachoweza kufanywa." Kasema, "Hebu nizungumze na mhubiri huyo."

Kasema, "Vema." Naye akampa namba yangu.

Akapiga simu, nilikuwa huko nje, kasema, "Ninii… " na kumwambia mke wangu, nimpigie.

167 Nilipiga simu siku nzima Jumamosi, na usiku kucha—kucha, na hadi kufikia saa sita Jumamosi usiku, kamwe hakuipokea. Niliona alikuwa akinikwepa, mnaona, kunizuia nisije huko.

Ndipo Ndugu Huff akapiga simu, kasema, "Ndugu Branham, watamhamisha Jumatatu."

Nikasema, "Hebu nikwambie, Ndugu Huff, yeye hanijui, kwa hiyo nipokee humo kama mgeni, hebu niruhusu tu niingie kama mgeni."

168 Naye akasema, "Vema." Kwa hiyo kesho yake akaja kunichukua kama mgeni. Na ninii…wake…pacha, mmoja wa hao mapacha, na yule msichana mwingine mdogo wakaingia kwenye gari kwenda kule pamoja nami. Tukavuka mto, na kwa hiyo mama na baba wakatangulia.

169 Ndipo nikaanza kuwahoji hao wasichana. Kasema, "Unajua, jambo la kuchekesha sana, Ndugu Branham," kasema, "asubuhi ya leo," maskini mtoto huyo wa kupendeza, akasema, "unajua, mchungaji wetu alisema, alianza kuhubiri juu ya jambo fulani, naye akabadilisha somo lake na kuanza kuzungumza juu ya uponyaji kwa mafuta." Kisha kasema, "Baba, mama alianza kulia kwa sababu, nasi tukalia pia, kwa sababu tulijua ulikuwa . . . kuja kukuchukua." Kasema, "Kuna namna fulani ya uponyaji ambao watu hufanya katika Biblia, kwa mafuta."

Nikasema, "Uh-huh, Dada," nikasema, "Ninajua unachozungumzia."

170 Akasema, "Unafikiri hilo lingeweza kuwa linahusu, kwamba Mungu alikuwa akijaribu kutuambia kupitia kwa mchungaji wetu juu ya jambo ambalo tungebahatika kwa njia hiyo?"

Nikasema, "Tutaona tutakapofika kule, na kuona kile Roho Mtakatifu asemacho."

171 Nao walipoufungua mlango, mwajua, wanaufungua mlango kisha wanaufunga nyuma yako, wanafungua lifti na kukupeleka juu, kisha wanaifunga tena, unajua, kuwazuia watu, wanakuweka kwenye seli.

172 Ameketi pale, maskini msichana mrembo, mwenye umri wa miaka kumi na minane, maskini kipenzi, mrefu *hivi*, macho makubwa, mazuri, laini, ameketi pale, ninii tu—ninii tu, loo, katika hali mbaya sana, namna hiyo tu. Nami nikasema, "Unanikumbuka, Margaret?"

Kasema, "Loo, loo, loo!"

173 Nami nikasema, "Mimi ni Ndugu Branham, hivi hunikumbuki? *Billy* ulizoea kuniita, kule chini, nami ningeninii . . . Ulipokuja, ulikuwa kama mbegu ndogo ya malenge, msichana mdogo, mara ya mwisho nilipowaona ninyi nyote, maskini nguo fupi namna *hiyo*. Hivi hunikumbuki."

Kasema, "Loo!" macho makubwa mno, mwajua, yakionekana namna *hiyo*.

174 Nikawaza, "Ee Mungu!" Niliketi na ninii yangu, kwa namna fulani niliweka tu mguu wangu mwishoni mwa kitanda. Kulikuwako na mwanamume aliyeketi pale akijaribu kumshika mke wake, alikuwa katika hali mbaya sana. Msichana huyu aliyeketi hapa, naye baba alikuwa amesimama karibu na huyo msichana, mama yake aliketi kwenye kona nyingine ya kitanda. Tulikuwa tumeketi pale, nikaendelea kushangaa, "Bwana, utasema jambo fulani? Utasema jambo fulani."

Nikasema, "Hunikumbuki, Margaret?" Naye alipoendelea tu kuniangalia, asingeweza kutambua chochote.

175 Kasema, "Ndugu Branham, yeye, jambo pekee analoendelea kuzungumzia ni kuhusu damu, na kwenye barabara kuu, na mambo kama hayo," kasema, "mambo ya ajabu ajabu sana."

Nami nikasema, "Jambo hili limekuwa likiendelea kwa muda gani?"

Kasema, "Miaka miwili."

176 Nami nikaendelea kuzungumza naye. Loo, lakini neema ya Mungu! Katika dakika chache tu Roho Mtakatifu akaanza kuingia. Nikasema, "Margaret, hunijui, lakini," nikasema, "maishani mwako mwote, tangu umekuwa mkubwa vya kutosha kujua kuhusu wavulana, sikuzote ulikuwa na fununu moyoni mwako utaolewa na mhubiri, ulitaka kuolewa na mhubiri." Ndipo akaanza kutabasamu, hilo likashika, mnaona, niliona Roho Mtakatifu alikuwa nalo. Ndipo basi nikasema, "BWANA ASEMA HIVI, imekwisha." Nikawaza, "Nilisema nini?"

177 Wengi wenu mmesoma kuhusu wale kuchakulo, na kadhalika. Nikasema, "Imekwisha." "Vema," nikawazia, "kama Yeye alisema hivyo, ninadumu moja kwa moja nalo." Nikasema, "Ndugu Huff, sijui ni kwa nini nilisema hivyo, siwezi kukwambia." Nikasema, "Nililisema tu, na hilo tu ndilo ninalojua, nililisema tu." Nami nikasema, "Lakini angalieni tu, katika saa chache zijazo kutakuwa na badiliko humu ndani." Hiyo ilikuwa yapata saa kumi na moja alasiri. Nikasema, "Kutakuwa na badiliko kubwa hapa katika saa chache zijazo!"

178 Ndiyo kwanza nizungumze habari zake asubuhi hiyo kanisani, huko chini maskanini. Nadhani baadhi ya watu wa maskanini hapa sasa, Fred Sothmann, na hao wengine niwajuao walikuwa hapa, ambao, ama, hao huko chini waliosikia hayo yakisemwa. Loo, ninaamini wavulana hawa walioketi papa *hapa* walikuwa kule. Ni wangapi humu ndani wanaokumbuka nikisema huko maskanini? Naam, wako hapa. Mnaona? Nikasema, "Iweni katika maombi," nikasema, "jambo fulani liko karibu kutukia, jambo fulani liko karibu kutukia."

179 Ndipo niliporudi nje, nilitoka nje ya . . . waliifungua milango na kuniruhusu nitoke, na ndipo nilipoingia kwenye gari na kuendesha kuizunguka hiyo kona, nikasema, "Baba wa Mbinguni, kwa nini nikasema hivyo? Kwa nini nikasema hivyo?" Si zaidi ya vile ilivyokuwa wakati niliposema kwa hao kuchakulo, na kadhalika, nao wakatokea. Nikasema, "Jambo fulani liko karibu kutukia." Ilithibitishwa tena hapa kwenye mkutano uliofuata, huu wa mwisho namna hiyo, kile kilichokuwa karibu kutukia.

180 Basi nilipofika nyumbani, nilibadilisha tu nguo zangu, nilikuwa nikirudi kanisani, Ndugu Huff akanipigia simu, akasema, "Ndugu Branham, nisingeweza kulishikilia zaidi." Kasema, "Unajua nini? Baada ya wewe kuondoka, yapata nusu saa baada ya wewe kuondoka, madaktari waliingia." Kasema, "Margaret alikuwa ameketi kitandani . . . "

181 Basi nilipokuwa nimeketi pale, basi nikasema, "Margaret, ni BWANA ASEMA HIVI, imekwisha," naye mama yake akanipiga

tu kwenye go—goti namna *hiyo*, naye akampigia kelele binti yake, bila hata kujua alichokuwa akifanya, naye akasema, “Mpenzi, kamwe hajapata kukosea,” namna hiyo, “kamwe hakosei.” Nami nikatoka nje ya jengo.

Bw. Huff akanipigia simu, kasema, “Ndugu Branham, madaktari waliingia hapa ndani, na kusema, ‘Imekuwaje?’ Kasema, ‘Kwani huyu msichana amejirudia!’”

182 Kasema, “Tutampeleka nyumbani kesho, ameruhusiwa kuondoka, yeye ni mzima na mwenye afya kama mtu yeyote angeweza kuwa.” Yuko nyumbani usiku wa leo, akishangilia. Kwa sababu gani? Kulikuwa na sauti inayojulikana. Haidhuru ni kitu gani kilicho kinyume, ni sauti ya hakika. Loo, Mungu, sauti hiyo ya hakika!

183 Mbili au tatu tu zaidi, kama dakika tano zaidi. Sauti ya hakika, jinsi tungeweza kuendelea! Jambo fulani lilitukia barabarani hivi majuzi, jambo lile lile, linaendelea tu kuingia, zaidi na zaidi, zaidi na zaidi, zaidi na zaidi. Kwa nini? Ni sauti ya hakika, kwa sababu kule mwituni siku hiyo, Ndugu Fred, Ndugu Tom, na wengine wenu ninyi nyote hapa, Ndugu Leo, wewe, wakati mtu huyo . . . Malaika wa Bwana aliposimama pale mwituni, na kusema jambo hilo, “Nena Neno hilo na uliangalie likitendeka,” hiyo haikuwa sauti isiyojulikana, hiyo ilikuwa ni *sauti*, ninajua ni ya Kweli. Ninaamini hilo, mimi . . . kwa moyo wangu wote, Biblia hii ikiwa juu ya moyo wangu, ni Mungu. Tuko kwenye wakati wa mwisho.

184 Yesu, wakati alipokuwa duniani, hapakuwapo na sauti isiyojulikana Kwake. Alisema, “Ninao uweza wa kuutoa uhai Wangu, ninao uweza wa kuutwaa tena.” Hakuna mashaka juu ya hilo, ilikuwa ni sauti ya hakika. Kwa nini? Alikuwa amesikia kutoka kwa Mungu. Sawa. Haleluya! Sasa najisikia kupaza sauti. Ninajisikia wa kidini sasa. Sasa, tunashuka kutoka upande wa hasi kuingia kwenye sauti chanya, ya hakika.

185 “Kama baragumu ikitoa sauti isiyojulikana ni nani anayeweza kujiandaa?” Lakini baragumu inalia, tuko kwenye wakati wa mwisho, inaambatana na Maandiko, “Itakuwa Nuru wakati wa jioni. Ishara hizi . . . ” na kadhalika. U—upo hapa. Baragumu inatoa sauti ya kweli, hebu na tujiandae. Hiyo ni kweli, hebu na tuwe tayari, jambo fulani liko karibu kutukia, ndugu, dada.

Yesu alisema, “Nina uwezo wa kuutoa uhai Wangu, ninao uweza, kuutwaa tena.”

Sio, “Labda nitakuwa nao. Natumaini ninao.”

Alisema, “Ninao.” Amina. Jambo ndilo hilo.

186 Wakati Martha alipotoka kwenda kumlaki wakati Lazaro alipokuwa amekufa siku nne, kasema, “Bwana, kama

ungalikuwa hapa ndugu yangu asingalikufa, lakini hata sasa lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa":

Yesu alisema, "Mimi ndimi Ufufuo na Uzima."

Sio, "Natumaini ndivyo nilivyo."

187 "Mimi ndimi." Amina. "Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Na kila aishiye na kuniamini Mimi, hatakufa kamwe. Je, unasadiki haya?" Hakuna mashaka kuhusu hilo. "Mimi ndimi."

"Nitakuwa. Natumaini kuwa."

"Niko sasa, nilikuwako daima, na daima nitakuwako. Mimi ndimi Ufufuo na Uzima. MIMI NIKO, MIMI NIKO." Naam. Hakuna mashaka yoyote kuhusu hilo.

"Mmemweka wapi?" Amina.

Sio...Sitaninii...Sasa, si, kumbukeni, "Nitaenda nione kile ninachoweza kufanya juu yake."

188 "Nitaenda na kumwamsha." Hakuna mashaka kuhusu hilo. Ndivyo ilivyokuwa, hakika. Kwa nini? Mungu alikuwa amemwambia hivyo. Hiyo ni kweli. "Sifanyi neno mpaka Baba Yangu anionyeshe kwanza." Yohana Mtakatifu 5:19, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda. Kile afanyacho Baba Yeye humwonyesha Mwana." Amina. Hakuna mashaka kuhusu hilo.

189 "Amekufa, anaozea kaburini, lakini ninaenda kumwamsha." Amina. "Ninaenda kumwamsha." Hakuna mashaka katika hilo...Kumbukeni ya kwamba "Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi." Hakuna mashaka kuhusu hilo, hilo ni kweli kama vile Mungu alivyo wa kweli. Loo, hivi huna furaha kwamba Yeye anakujua? Hivi huna furaha kwamba jina lako liko kwenye Kitabu Chake? "Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi." Amina. *Whiu!*

190 "Mimi ndimi Ufufuo na Uzima," nami niko ndani Yake. Mungu alithibitisha kwa kumfufua, Yeye atanifufua mimi pia. Tayari nimeketi katika mahali pa Roho, nimefufuka. Ndivyo ilivyo kulingana na Mungu. "Wale aliotangulia kuwajua, aliwaita; wale aliowaita, aliwahesabia haki; wale aliowahesabia haki, amewatukuza." Amina. Sasa hivi, katika—katika hatua ya kutukuzwa, wameketi katika mahali pa Roho katika Kristo Yesu, katika hali ya utukufu, huku nguvu za ufufuo zikiwa ndani yetu zimetubadilisha kutoka mwenye dhambi tukawa Mkristo. *Whiu!* Hakuna mashaka hapo, hakuna mashaka.

191 "Unajuaje?" Anaishi ndani yangu. Unajuaje? Yuko ndani yako. Amina. Hiyo ndiyo sababu mambo haya yanatendeka. Hakuna mashaka juu yake, tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani kwa sababu tu hai. "Yeye aliyekuwa amekufa, ajaponiamini Mimi, hata hivyo ataishi. Naye kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe." Wote wanaomwamini na

kumjia, "Nitampa Uzima wa Milele." Sasa hivi, tuna Uzima wa Milele na tutafufuliwa katika siku za mwisho. *Whiu!* Jamani, jambo ndilo hilo. Hakuna mashaka kuhusu hilo. La, tayari imefanywa.

192 "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipoitwa na Baba Yangu. Na wote alionipa Baba watakuja Kwangu." Ni wangapi walio Wakristo, inueni mikono yenu? Vema, tayari mko katika hali ya utukufu. Amina. "Wote alionipa Baba watakuja. Wala wote wajao sitawatupa nje kamwe; nitawapa Uzima wa Milele, na kumfufua katika siku ya mwisho. Nitamfufua."

"Labda nitamfufua."

193 La, "Nitafanya hivyo." Hiyo ni sauti ya hakika. Hiyo ni ya hakika. Tutafufuka katika hali ya utukufu. "Huu upatikanao na mauti utakapovaa kutokupatikana na mauti, uharibikao uvae kutokuharibika." Hakuna mashaka. Tunaogopa nini? Loo, haleluya! Hakuna cha kusisimua, hakuna cha ku—kuogopa, namaanisha. Loo, jamani, kwa nini? Hakuna mashaka, tuna hakika.

194 "Nitamfufua. Huu upatikanao na mauti utakuwa. . .utavaa kutokupatikana na mauti. Haijadhihirika bado tutakuwa na mwili wa namna gani, bali tunajua tutakuwa na mwili kama mwili Wake Mwenyewe wenye utukufu, kwa kuwa tutamwona jinsi alivyo." Amina. Hakuna mashaka juu yake. "Tutamwona." Utukufu! Hakuna mashaka, yote ni ya hakika.

195 Loo, unaweza kuendelea na kuchukua sauti hiyo isiyojulikana ukitaka, bali ninapenda baragumu ya Injili inayotoa sauti inayojulikana. Baragumu ya Injili ni nini? Habari njema. Hiyo ni kweli. Yuko hapa sasa. Sasa, hakuna mashaka juu yake. Vema.

196 Hakusema, "Nitashuka niende nione kile ninachoweza kufanya kuhusu Lazaro. Nitashuka niende nione kile ninachoweza kufanya. Nitashuka niende nijaribu kuona kama ninaweza kumfufua." "Atafufuka tena." Hiyo ni hakika, chanya.

Vema, unasema, "Sasa, ukizungumza juu ya Yesu, ulikuwa ukizungumza juu ya Ibrahimu, na wewe je?"

197 Naam, tuna uhakika, pia. "Bado kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi." Hiyo ni hakika, uhakika, "Nitakuwa."

"Labda nitakuwa. Huenda ikawa nitakuwa."

198 La, "Nitakuwa." Hilo ni hakika. "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu." Unaweza kusema ni ulokole ukitaka, lakini ni sauti ya hakika kwangu kwamba nimeokoka. Amina. "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata ukamilifu wa dahari." Hiyo ni hakika kwamba utajua.

"Unajuaje kwamba una hakika?"

199 Vema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Hiyo ni ishara. Nitawapa ishara kuthibitisha—kuthibitisha ya kwamba niko pamoja nanyi. Haitakuwa na mashaka . . .

Unasema, "Vema, jamani, nitajuaje kama nina mhemuko ama sina, kama nimechochewa tu ama la?"

"Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Hakuna mashaka.

200 "Tunajuaje kama sisi ni Wakristo au la? Sasa, tunaenda ulimwenguni kote na kuihubiri Injili, na tunabatizwa, na kadhalika, tunajuaje kwamba sisi ni—sisi ni Wakristo?"

"Ishara hizi zitafuatana na hao, nitawapa uhakika, sauti ya hakika, ishara ya hakika."

201 Vema, hivi ndivyo itakavyokuwa: Mhubiri anasema, "Njoo, ujiunge na kanisa letu, kisha ukariri kanuni yetu ya imani, ama ubatizwe, ama kunyunyiziwa, ama kumwagiliwa," ama, loo, chochote kile, unaona, "na hilo—hilo latosha." Yesu kamwe hakusema lolote kuhusu hilo. Hiyo ni sauti isiyojulikana.

202 Unasema, "Vema, mama yangu alikuwa mfuasi wa kanisa hili." Hilo ni zuri sana. "Vema, na—nawaambia, nilienda kule na kupewa kipa imara." Hilo—hilo—hilo ni sawa, pia, lakini hilo—hilo—hilo si . . . hilo bado halina uhakika. Hmm!

203 Yesu alisema, "Nitawapa ishara ya hakika. Ishara hizi . . . " Marko 16, Maneno ya mwisho aliyoliambia Kanisa Lake, "Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." Umbali gani? Ulimwenguni kote. Wangapi? Kila kiumbe. Si kitu kama misheni . . . na mamilioni, na mabilioni, na mabilioni bado hawajaguswa. Mnaona? Sasa, Ye—Yeye alisema . . .

"Vema sasa," wanasema hivyo, "iliishia kwa wale wanafunzi."

204 La, la. Hii hapa sauti ya hakika: "Ulimwenguni kote, na kila kiumbe." Hilo ni la hakika. Wakati Injili inapohubiriwa, "Ishara hizi *zitafuata*!"

Sio, "Labda zitafuata. Zinapaswa kufuata."

"Zitafuata!" Hilo ni la hakika. Loo! Loo, ndugu, nina furaha kuwa Mpentekoste moyoni. Naam, bwana.

205 "Loo, ishara hizi *zitafuata*!" Ni hakika. "Ishara hizi hakika zitafuatana na hao waaminio, katika Jina Langu watatoa pepo, watanena kwa lugha mpya, kama wakishika nyoka au kunywa kitu cha kufisha hakitawadhuru, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Ishara za hakika.

"Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu . . . "

"Unajuaje tuko katika wakati wa mwisho? Itakuwaje wakati wa mwisho, Bwana? Vema, tunajuaje tuko kwenye wakati wa mwisho?"

"Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa."

"Ndivyo *itakavyokuwa*!"

Si, "Labda itakuwa." Ama, "Inapaswa kuwa wakati huo."

206 La, "*Itakuwa*," Roho yeye yule, akiishi katika mwili wa mwanadamu, akiyatambua mawazo ya moyo, kasema ni nani aliyekuwa nyuma Yake, mnajua ninalomaanisha. Tuko kwenye wakati wa mwisho. "*Itakuwa* kama ilivyokuwa katika siku za Lutu." Mtu fulani hana budi kusimama, kitu fulani hakina budi kufanya hivyo.

207 Lakini pia ilisema katika wakati wa mwisho yale, jinsi kanisa litakavyokuwa vuguvugu, lianguke. Itakuwa, hakuna haja ya kujaribu kulikomesha, itakuwa hivyo. Lakini kuna wengine mle ndani, Yeye alisimama, wakati pekee wa kanisa wa zile nyakati saba za kanisa, Laodikia ndiko ambako Yesu alionekana nje ya Kanisa Lake, akibisha mlango, akijaribu kurudi ndani. Hiyo ni kweli, wakati pekee wa kanisa. Naam, bwana. Katika Laodikia, wakati wa kanisa la Kipentekoste, *unavyojiita*, walikuwa wameunda kanuni nyingi sana za imani na madhehebu hata mkamtoa Yesu nje, Naye alikuwa amesimama mlangoni akibisha. [Ndugu Branham anabisha mara kadhaa—Mh.]

208 "Wote niwapendao, Mimi huwakemea na kuwarudi." Sasa, msinikasirikie ninapowaambia, mnapaswa kuacha nywele zenu zikue, na kuacha kuvuta sigara, na—na kuacha kuvaa kaptura, na kufanya mambo haya yote ya namna hii, na mwishi jinsi Wakristo wanavyopaswa kuishi, mnaona, "Wote niwapendao, ninawarudi na kuwakemea, iweni na bidii na mtubu." Yale aliyosema. "Naye atakayeufungua mlango na kuniruhusu niingie, nitaingia na kula pamoja naye, naye pamoja Nami. Nitaingia, ikiwa tu utafungua mlango." Sio, "labda nitaingia, nitalitafakari," "nitaingia. Nitaingia kwa kila mtu atakayefungua mlango." Loo, hizo sauti za hakika. Ninapenda hilo nanyi je? Naam, bwana.

Unasema, "Vema sasa, Ndugu Branham, nakwambia nililofanya. Ni—nilienda na kujiunga na kanisa, naamini sasa, ya kwamba niliokoka."

209 Hivyo sivyo ilivyo. Huh-uh. Petro alisema kwenye siku ya Pentekoste, kasema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe kwa Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtampokea Roho Mtakatifu."

La—la, "Ninyi, labda mtampokea."

210 Hakuna—hakuna *labda* kuhusu hilo. "*Mtapokea*, kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, kwa watoto wenu," na kwao huko Middletown, au, "wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Ni hakika.

211 "Na wote waliompokea, aliwapa uwezo," (Utukufu kwa Mungu!) "kuwa wana wa Mungu." Wana, wote walioamini waliongezwa kwa Kanisa. Unaingiaje Kanisani? "Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja." Hakuna mashaka juu yake, ni hakika, sauti ya hakika.

Hivi nimetumia kanda mbili ama tatu hapa nje, Leo? Nitamalizia. Nitawaweka tu hapa, nusu usiku. Loo, jamani!

212 Waebrania 13:8, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Hiyo ni kweli? "Atakuwa sehemu ya njia. Ye—Yeye atakuwa baadhi ya ni—ninii . . . " "Atakuwa yeye yule," hakuna mashaka kuhusu hilo, sivyo? La hasha. Vema.

213 "Yeye aniaminiye Mimi, yuna Uzima wa Milele." Hakuna mashaka kuhusu hilo. "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa Milele." Hakuna mashaka kuhusu hilo. Hiyo ni kweli? Ni ahadi ya Mungu. Toba kwa Mungu, na kujazwa na Roho Mtakatifu, uponyaji wa Kiungu, na mambo hayo yote ni ya hakika, ni ahadi za Mungu. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

214 Sasa, mnasema, "Ndugu Branham, mimi ni mfuasi wa Assemblies." Hilo ni zuri. Ni sawa kwangu kuwa mfuasi wa Assemblies au kanisa lolote, ni kanisa zuri. Mojawapo ya wadhamini wangu wakuu sana ni Assemblies of God.

215 "Mimi ni mfuasi wa Church of God." Vema, sawa, nami, pia, wa Church of God, nami ni mfuasi wa Assemblies, pia. Mnaona? Na, Church of God, mojawapo wa wadhamini wangu wakuu.

216 "Mimi ni mfuasi wa Foursquare," unasema. Vema, nami, pia. Mnaona? Wao ni kanisa zuri, mi—mi—mimi . . . kundi zuri la watu. Kuna Kanisa *moja* tu katika hayo yote, yote pamoja ni kama Kanisa; lakini hilo, makundi hayo ni mazuri. Mnaona?

217 "Mimi ni mfuasi wa United." Hakika, ni mfuasi, pia. Mnaona? Ni ndugu wazuri, wazuri. Mnaona? Vema. Mimi ni mfuasi wao, pia. Mimi ni wao, kwa sababu niko katika Kanisa lile lile walilomo. Kila mtu aliyejazwa na Roho Mtakatifu, kwa sababu kwa Roho mmoja sote tulibatizwa kuwa Mwili mmoja. Hiyo ni kweli? Sasa, hiyo—hiyo—hiyo si sauti isiyojulikana, hiyo ni Wakorintho wa Kwanza mlango wa 12, "Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja, na kuwa washiriki wa Mwili huo." Amina.

218 Sasa, jambo ndilo hili: Siku hiyo, Yesu alisema atawatenganisha kondoo na mbuzi, aliahidi ya kwamba kungekuwako na ko—ko—kondoo na mbuzi, na ninii . . . Naye aliahidi kungekuwako na mwa—mwanamwali mwenye busara na mwanamwali aliyelala. Watakuwako, kila kitu asemacho ni hakika. Nami ni—nina furaha sana, usiku wa leo, kujua ya kwamba—ya kwamba bila shaka yoyote, nimezaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu. M—m—mnapenda hilo? Mnaamini hilo?

219 Sasa, hapo ndipo ninaposimama, kama tu. . .Na kutoa tamshi hili katika kufunga. Paul Rader, ra—rafiki yangu, nimemnukuu dakika chache zilizopita katika kifo chake, alipokuwa akienda. Paul Rader alisema, wakati mmoja, kwamba alizoea, alitoka Oregon, huko ndiko makazi yake yalikokuwa, naye alikuwa akikata miti. Naye alisema wakati mmoja yeye, bosi wake, naye alikuwa katika ndoto, naye bosi wake akamtuma kwenda kukata m—m—mti fulani katika ukubwa fulani. Ba—basi akaukata huo mti, naye akaweka tu shoka kwenye hilo gogo.

220 Nayo misuli iliyo mikubwa zaidi ya mwanamume iko mgongoni mwake, lakini anapoanza kuinua, yeye huinua kwa miguu yake, mikono, mgongo, ana nguvu zaidi mgongoni mwake kuliko sehemu yoyote ya mwili wake. Kwa hiyo, akalishika hilo gogo, na kuweka magoti yake pamoja, naye akang'ang'ana tu, na kung'ang'ana, na kung'ang'ana, na kung'ang'ana, mpaka kwa kweli asingeweza kwenda mbali zaidi. Alijichosha tu, kasema, "Nilikuwa nimedhoofika sana, hata nisingeweza kusogea, nilikuwa dhaifu sana."

221 Na yale yaliyokuwa yakitukia, alikuwa akifanya umishenari ng'ambo. Alikuwa huko nyuma kabisa, na kuna wingi wa ninii, wanayoita, homa ya maji meusi, nafikiri hiyo ndiyo Paul aliugua. Hakuna daktari karibu, popote, naye Paul alikuwa mwaminio mashuhuri katika uponyaji wa Kiungu, kama nyote mlijua jambo hilo, naye alikuwa, mtu mashuhuri.

222 Billy Sunday alikuja Chicago wakati mmoja kuhubiri mikutano michache huko na. . .katika Maskani ya Injili ya Chicago, na—na kwa hiyo, Paul alikuwa huko juu akihubiri. Basi Billy akahubiri yapata juma moja ama siku kumi, naye akaishiwa na mahubiri, hakuwa na mahubiri mengine, naye Paul alikuwa akihubiri kwa yapata miezi sita ama minane huko, ndipo akamwambia Paul, kasema, "Paul, kwani unaishiwa na mahubiri lini?"

223 Kasema, "Mpira wangu wa maji unapopasuka." Kwa hiyo, ali—alikuwa anaenda kuninii. . .Kwa hiyo, huyo—huyo alikuwa ni Paul. Kwa hiyo, yeye, mpira wake wa maji ulipopasuka, mwajua, alisimamishwa, jambo fulani alilofanya, kitu fulani kikaukatiza umeme, mnaona. Alisema alienda tu mimbarani. . . Na ninyi nyote, mtu yeyote aliyewahi kumjua Paul Rader, angeanzia katika Mwanzo na kuhubiri hadi Ufunuo, na kote katika Biblia, na popote pale, alisimama tu pale na kuanza kupigapiga mpaka akayafikia mahubiri, na akaanza juu yake.

224 Na kwa hiyo, a—a—akashikwa na homa hii ya maji meusi, naye, nao walidhani alikuwa yuafa, ndipo akamwambia mke wake, kasema, "Simama karibu nami, uombe." Hicho chumba kikaendelea kuingia giza, hatimaye kikawa giza tupu, hapo ndipo alipoota ndoto hii. Naye akasema ya kwamba a—alibahatisha ilikuwa ni nini, ilikuwa tu kwamba homa hiyo

ilimlemea kabisa, mpaka akawa tu amekwisha. Nanyi mnajua homa ya maji meusi ni nini, huishi na hiyo. Kwa hiyo, alikuwa amemwamini Mungu, akamtumainia Yeye wakati wote. Kwa hiyo a—alimwambia mke wake aombe, huku amemwekea mikono, na kuomba. Nao iliwabidi watoke kwa mtumbwi siku baada ya siku wapate kutoka mahali walipokuwa.

225 Ndipo basi kasema, mmoja . . . Aliota kwamba aliling'ang'ania gogo hili, mpaka akachoka kupindukia, akasema alininii tu, nguvu zake zilikuwa zimekwisha kabisa. Kasema alichoka sana, akaketi tu chini, akaegemea mtini, ndipo akasema, "Nimekwisha. Kamwe siwezi kuliinua gogo hilo, ni . . . Kwani Nguvu zangu zote zimeenda wapi? Mbona, ningeweza kuinua gogo hilo na kuliweka mgongoni mwangu kwa mkono mmoja," kasema, "niondoke hapa," kasema, "mti mdogo." Naye alikuwa ni mtu mwenye nguvu sana. Basi akasema, "Ningeweza . . . Mbona, nimeinua miti mikubwa kuliko huo wakati wowote, nikaenda nayo." Naye akasema alikuwa tu ameketi pale, ndipo akaanza tu kulia. Akasema, "Nguvu zangu zote zimekwisha, siwezi kufanya jambo lingine, nguvu zangu zimekwisha."

Naye akasema alimsikia Bosi wake akipanda juu, na kusema, "Paul, kuna nini?"

226 Naye akasema alidhani ya kwamba Bosi alikuwa na Sauti tamu sana aliyopata kusikia. Naye akasema, "Ni—ni—nimekwisha. Si—sina nguvu tena, siwezi kwenda mbele zaidi. Siwezi kuliinua hilo gogo, kamwe siwezi kuondoka nalo."

227 Akasema, "Paul," Yeye akasema, "kwa nini unapambana nalo, kwa vyovyote vile?" Mnaona? Akasema, "Kile pale kijito kikibubujika, kikipitia papo hapo karibu nawe." Kisha kasema, "Mbona usilitupe tu kwenye hicho kijito pale, halafu upande juu yake na kushuka chini? Kambi iko chini tu ya kilima, ushuke moja kwa moja kwa viwimbi hadi kambini." Kasema, "Lifingirishe tu kijitoni, kisha ulirukie. Liendeshe huko chini, acha likubebe ushuke."

228 "Vema," akasema, "Sikuwazia hilo kamwe." Kisha kasema, "Alipogeuka, aliona Bosi wake alikuwa ni Nani, ilikuwa ni Bosi wake *halisi*." Kasema alilisukuma majini, akalirukia akatagaa juu ya hilo gogo, na kusema alifurahi sana, akaanza kurusha maji namna *hiyo*, na kupiga makelele, "Nimepanda juu yake! Nimepanda juu yake! Nimepanda juu yake!" Akienda juu ya hivyo viwimbi, vizuri tu, akienda mbio kambini namna *hiyo*, akipaza sauti, "Nimepanda juu yake!"

229 Ndipo kasema alipojirudia, aliruka moja kwa moja katikati ya sakafu, mke wake amelala hapo pembeni ambapo ndiyo kwanza amrushe, huku akipiga mayowe kwa sauti yake yote, akisema, "Nimepanda juu yake! Nimepanda juu yake! Nimepanda juu yake!"

230 Ndugu, hivyo ndivyo ilivyo, usiku wa leo. Siku moja niligundua kwamba Yesu Kristo alinipenda, nikatambua ya kwamba nilizaliwa nipate kuwa mtoto Wake, akaniita, na kunipa Uzima wa Milele. Sijui kifo changu kitakuja lini, sijui, haijalishi kwangu. Lakini kuna jambo moja la hakika: Kila Neno aliloahidi katika Kitabu hiki, nimepanda juu Yake! Nimepanda juu Yake! "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni kwa ajili ya yeyote atakaye, atakuja na kuupokea; uponyaji wa Kiungu ni kwa ajili ya kila mtu, yeyote atakaye anaweza kuja na kupokea baraka yoyote.

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
Ambamo wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya hilo gharika,
Wanapoteza madoa yao yote ya hatia.

Yule mwizi aliyekuwa akifa alifurahi kuona
Chemchemi hiyo katika siku zake;
Hapo naomba mimi, ingawa ni mwovu kama yeye,
Nioshe dhambi zangu zote.

Tangu wakati huo kwa imani nilipokiona hicho kijito
Kinachotokana na majeraha yako,
Upendo wa kukomboa umekuwa ndio mada yangu,
Na utakuwa hata nitakapokufa.

Kisha katika wimbo mzuri, mtamu zaidi,
Nitaimba nguvu Zako za kuokoa,
Wakati maskini ulimi huu wenye kithembe, unaogugumiza
Utakapolala kimya kaburini.

231 Nimepanda juu yake, ndugu, nimepanda juu yake. Nilikuja kwa Wapentekoste, walikuwa na madhehebu mbalimbali, kama tu Wabaptisti walivyokuwa nayo, kamwe sikujiunga na yoyote yao, nilisimama moja kwa moja katikati ya makundi hayo, nami nilijua walikuwa ni ndugu katika yote mawili, makundi yote yaliyo karibu, nikamkumbatia kila mmoja wao namna *hiyo*, nao ni ndugu zangu. Nimepanda juu yake.

232 Hivi majuzi huko Beaumont, Texas, kundi fulani la watu, kanisa la kimadhehebu lilikuwa na makanisa sabini na mawili yakidhamini mikutano yangu, nao walikuwa na mkutano mkubwa ukiendelea. Nilikuwa na ndugu aliyeketi mimbarani, jukwaani, ndi—ndipo mzee wa wilaya akanipigia simu siku hiyo, naye akasema, "Nachukizwa na jambo hilo, Ndugu Branham, ulikuwa na mtu jukwaani aliyebatizwa vibaya." Kasema, "Ungewezaje kufanya hivyo?"

Nikasema, "Kwa nini?"

Akasema, “Vema, ye—yeye si mmoja wetu, ha—ha—hawezi kuwa.”

Nikasema, “Vema, yeye ni ndugu yangu.”

233 Akasema, “Unajua kile tumefanya?” Kasema, “Tumechora mstari mdogo, na kukukatilia mbali kutoka miongoni mwetu.”

234 Nikasema, “Sasa, nitachora mstari mdogo juu ya wenu, na kuwarudisha ndani tena,” nikasema, “Nawarudisha tena. Mbona, wewe ni ndugu yangu!” Nimepanda juu yake. Sijali wanachoamini, ninaamini ya kwamba Yesu Kristo hajagawanyika, “Sote ni Mwili mmoja; mmoja katika tumaini na Mafundisho, mmoja katika upendo.” “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Nimepanda juu yake.

235 Je, mngetaka kupanda juu yake, usiku wa leo? Je, wewe ni mgonjwa? Je, wewe ni mhitaji? Kuna mwenye dhambi hapa angesema, uinue mkono wako, useme, “Niombee, Ndugu Branham, ninataka kupanda juu ya ahadi ya Mungu, ‘Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele,’ ninataka kupanda juu yake, ninataka kuchukua msimamo wangu sasa hivi”? Inua mkono wako, useme, “Niombee.” Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hilo ni sawa. Mungu akubariki.

236 Mtu yeyote hapa asiye na ubatizo wa Roho Mtakatifu? Sema, “Ndugu Branham, najua hiyo ahadi ni yangu, Yeye aliniambia mle katika Matendo 2:38, kama nikitubu na kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, ondoleo la dhambi, ninapaswa kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Alisema katika Marko 16, ‘Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili. Aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini atahukumiwa. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.’ Mimi. . .Nimeahidiwa Roho Mtakatifu, nami ninamtaka, nami nitapanda juu ya hiyo ahadi mpaka Mungu atakaponipa.” Inua mkono wako, useme, “Mimi. . .” Vema, vizuri. Mungu awabariki.

237 Ni wangapi wenu hapa ndani, mnasema, “Mimi ni mgonjwa, Ndugu Branham”? Labda umepita tiba, sijui, kutoka kwa daktari. Hawezi kukutibu, anaweza kukusaidia, kukusaidia, mpaka Mungu akuponye. Lakini mimi. . .Kuna Tabibu mmoja tu, huyo ni Mungu. Kuna tiba, madaktari wana dawa, Mungu ana tiba, hivyo tu. Ana dawa nyingi, lakini kuna tiba moja tu, na hiyo ni kupitia kwa Mungu. “Mimi ndimi Bwana, niponyaye magonjwa yako yote.”

238 “Mimi ni mgonjwa, Ndugu Branham, nimejaribu kila kitu nijuacho, mimi, inaonekana kana kwamba siwezi kuushinda, lakini, usiku wa leo, Yeye ni Bwana aponyaye magonjwa yangu yote, alijeruhiwa kwa makosa yangu, kwa kupigwa Kwake mimi *nimeponywa*. Ninaliamini, nami nitapanda juu yake.

Ninainua mkono wangu, nikumbuke, Ndugu Branham, kwamba nitapanda juu ya ahadi Yake." Haleluya! Hii ndiyo.

239 Sasa, sikiliza, ewe rafiki, ninataka tu. . . Uwe mwaminifu kwangu. Hilo linawezaje kushindwa? Ninawauliza katika jina la akili timamu, hilo linawezaje kushindwa? Kama wewe ni mwenye dhambi na unamwomba Mungu akuokoe, Yeye aliahidi na hata akamtuma Kristo kufa upate kuokoka, unawezaje kushindwa kuokoka? Niambie ni wapi ungeweza kushindwa. Njia pekee ni kwa sababu uko *hapa* juu wala si *hapa* chini.

240 Kama ukisema, "Roho Mtakatifu ni wangu, nimetubu, nimekiri dhambi zangu, nimemwamini Kristo, nimebatizwa, niko tayari kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu," sababu pekee ya wewe kutokuwa naye, ni kwa sababu kuna kasoro *hapa* juu. Hiyo ni kweli. Huwazii ipasavyo. Kama alikuwa akitoka *hapa* chini, utampata sasa hivi.

241 Unasema, "Ndugu Branham, ninaamini katika uponyaji wa Kiungu, ninamkubali kama Mponyaji wangu. *Alijeruhiwa* kwa makosa yangu, kwa kupigwa Kwake mimi *nimepona*." Loo, ndugu. Hilo latosha. Ni hayo tu. Jambo pekee, kama iko *hapa* chini ni kweli, kama iko *hapa* juu, si kweli. Kama sivyo, basi Mungu aonekane kuwa mwongo, Yeye alitoa ahadi ambayo hawezi kuitimiza. Yeye huwatimizia wengine, na wewe je? Hiyo ni kweli? Liwazieni tu jambo hilo.

242 Unasema, "Ninataka Roho Mtakatifu." Yeye humpa yeyote atakaye. Hiyo ni kweli? "Ninataka kuokoka." "Kila aitiaye Jina la Bwana ataokoka." Hivyo ndivyo ilivyo. Mnaona, ni wewe, *hapa* juu, ni wewe, unayemwacha ibilisi atumie *hii*.

243 Hakuna mtu. . . Mungu anapofanya uamuzi, hauna budi kuwa ni uamuzi ule ule kila wakati, kama Yeye, kama ni kwa ajili ya jambo fulani unaloomba, kama Yeye alimwokoa mtu wa kwanza juu ya msingi wa imani, hana budi kumwokoa wa pili, akija, hana budi kuokoa kila mtu, ajaye. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Nimepanda juu yake. Ninaamini hilo. Je, unaamini kwa moyo wako wote. Simama kwa miguu yako basi.

244 Ninampa changamoto kila mwenye dhambi humu ndani, ninakuamuru, katika Jina la Yesu Kristo, kumwambia Mungu kwamba unasikitika kwa ajili ya dhambi zako, nawe unamkubali Yesu kama Mwokozi wako sasa hivi, uone kitakachotukia.

245 Ninampa changamoto kila mwaminio humu ndani ambaye ameokoka, kumkubali Kristo sasa hivi, kukujaza na Roho Mtakatifu, kuchukua yote, ukiri dhambi yako. Mwambie tu kwamba unasikitika, kwamba wewe. . .

246 Dhambi yako ni nini? Unasema, "Ndugu Branham, mimi tayari ni Mkristo." Kiri dhambi yako, dhambi yako ni kutokuamini, hiyo ndiyo dhambi pekee iliyopo, ni kutokuamini. Unaninii tu. . . Kutokuamini kwako kunakuweka mbali nao.

Kila mgonjwa humu ndani, kiri tu imani yako katika "mapigo Yake sisi tuliponywa," angalia kinachotukia.

247 Sasa, ni waaminio wangapi walio humu ndani? Inueni mikono yenu. Sasa, kama wewe ni . . . Sasa, unawajua hao watu wanaoinua mikono yao kama wenye dhambi, na yule waliokuwa. Ninataka kila mmoja wenu ninyi watu mweke mikono yenu juu ya mtu mwingine aliye karibu nawe, wekeaneni tu mikono, haidhuru mko wapi, huko juu jukwaani. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

. . . kama hawajakuwa, wanahitaji uponyaji, Bwana, achilia tu.

Ombeni.

248 Baba yetu wa Mbinguni, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, tunavunja uchawi, tunavunja kila nguvu za ibilisi, tunazivunja kwa imani, tunapodai haki ya Kristo. Ibilisi na aachilie kanisa hili, usiku wa leo, na atoke hapa, katika Jina la Yesu Kristo, kwa kuwa Damu ya Bwana Yesu Kristo imehubiriwa, na nguvu za Mungu zimefunuliwa.

249 Ibilisi, waachilie, toka, katika Jina la Yesu Kristo!

61-0315 Sauti Isiyojulikana
Full Gospel Tabernacle
Middletown, Ohio Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org